**BREAKING NEWS**
CHEZA SUPA JACKPOT
TZS 1,000,000,000
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**MABULA** awatuliza wabunge utendaji kamati mawaziri 8

UKURASA 8




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Mei 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580959

MWANGA WA JAMII


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## BAADA YA MISHAHARA

# Kicheko tena posho watumishi wa umma

UKURASA 2



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, jana ofisini kwake, Bungeni jijini. Viongozi hao walizungumza mambo mbalimbali ya ushirikiano baina ya taasisi hizo. **PICHA: BUNGE**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### BRELA YATAJA SABABU KUFUTA KAMPUNI 5,600

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umetangaza kusudio la kuanza kuzifutia usajili kampuni za kibiashara...

UKURASA WA 4

### VIWANDA VILIVYOTELEKEZWA VYAKABIDHIWA KUENDELEZWA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekabidhi kwa taasisi nne viwanda 10 ambavyo wawekezaji walishindwa kuviendeleza kulingana na...

UKURASA WA 4

### JELA MIAKA 20 KWA KUZINI NA BINTIYE

MKAZI wa Mtaa wa Kebikiri Rebu, Kata ya Turwa, Tarime mkoani Mara, Daniel Mgohi (53) amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela baada ya....

# Chongolo ashtukia mchezo mchafu uchaguzi wa CCM

UKURASA 3

# Dk. Hoseah arudi kwa kishindo TLS

UKURASA 2

**MICHEZO** KAZI MOJA TU LEO UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Dk. Hosea arudi kwa kishindo TLS

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MWANATAALUMA nguli wa sheria nchini, Dk. Edward Hoseah, ameshinda kwa awamu ya pili mfululizo Urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) baada ya kuwabwaga wapinzani wake kwa zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa jana jijini hapa.

Dk. Hoseah aliibuka kidedea kwa kupata kura 621 dhidi ya hasimu wake, ambaye ni Wakili maarufu Harold Sungusia aliyemfuatia kwa kura 380, huku Wakili Jeremiah Mtobesya akiambulia kura 145.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TLS, Wakili Charles Rwechungura, alimtangaza Dk. Hoseah kuwa mshindi wa uchaguzi huo, uliotawaliwa na mbwembwe za wagombea na wapambe wao kuelekea mchakato huo.

Aidha, wajumbe wa mkutano huo, wamemchagua Gloria Kalabamu kuwa Makamu wa Rais.

"Uchaguzi huu umefanyika kwa haki na tunashukuru Mungu, hakuna malalamiko. Tumezingatia uwazi na usawa," alisema Rwechungura.

Wagombea nafasi ya Makamu wa Rais, walikuwa watatu ambapo Gloria Kalabamu alipata kura 598, Angela Mbonde kura 449 na Nyachiringa Msalya, aliyepata kura 99.

Akizungumza baada ya kushinda Uchaguzi huo, Dk. Hoseah, alisema atahakikisha anasimamia uwazi, uwajibikaji na uwekezaji kwa kuendeleza mambo yote ili kufikia TLS ya uwekezaji.

Dk Hoseah aliwasihi mawakili wazoefu waliokimbia chama hicho cha wanataaluma, kurudi na kukaa na vijana kuwafundisha maadili ya kazi pamoja na kuwapa uzoefu.

"Serikali iliyopo madarakani kipindi hiki ni nzuri. Ni vyema tuitumie kuwekeza na si kuwekeza kama chama bali hata sisi kwa sisi mawakili wenyewe kwani TLS isiwe ni taasisi ya kuchukua fedha mifukoni mwa wanachama,"alisisitiza

Kwa mujibu wa Dk. Hoseah, mwelekeo wa sasa wa mawakili ni kuwekeza katika vitega uchumi.

Kutokana na kusudio hilo, alisema hivi sasa TLS inafikiria kutafuta fursa mbalimbali za kiuchumi.

# Kicheko tena posho watumishi wa umma

**Na James Mwanamyoto,** DODOMA

BAADA ya kupandisha mishahara ya watumishi wa umma kwa asilimia 23, Rais Samia Suluhu Hassan amepeleka kicheko kingine kwao, safari hii akitoa kibali cha kurekebisha posho ya kujikimu ya safari za ndani ya nchi kwa watumishi wa umma na kiwango cha malipo ya kazi maalum (Extra Duty).

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, utekelezaji wa kibali hicho umepangwa kuanza rasmi Julai Mosi, mwaka huu, yaani siku ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, alibainisha hayo jijini Dodoma jana wakati wa kikao kazi cha wakuu wa idara na vitengo vya utawala na usimamizi wa rasilimali watu katika utumishi wa umma chenye lengo la kutathmini utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dk. Ndumbaro alisema kuwa kutokana na kibali hicho cha Rais, posho ya kujikimu ya safari za ndani ya nchi kwa watumishi wa umma kwa kiwango cha juu imepanda kutoka Sh. 120,000 hadi 250,000 na kiwango cha chini kutoka Sh. 80,000 hadi 100,000.

Aliongeza kuwa kiwango cha malipo ya kazi maalum (Extra Duty) kwa watumishi wa umma kimeongezeka kwa ngazi zote, ambapo kwa ngazi ya chini kimepanda kutoka Sh. 15,000 hadi 30,000, kwa ngazi ya kati kimeongezeka kutoka Sh. 20,000 hadi 40,000 na kwa ngazi ya juu kimeongezeka kutoka Sh. 30,000 hadi 60,000.

Dk. Ndumbaro alisisitiza kuwa viwango hivyo vipya vitalipwa na serikali kupitia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hivyo taasisi zisiombe nyongeza ya bajeti ili kuwalipa viwango hivyo watumishi wake.

Kufuatia ongezeko hilo, Dk. Ndumbaro alitoa wito kwa watumishi wa umma wote nchini kufanya kazi kwa bidii, maarifa, weledi na nidhamu ya hali ya juu ili kuunga mkono vitendo jitihada za Rais za kuboresha maslahi yao. "Watumishi wa umma tuwajibike kwa hiari bila kushurutishwa, tuwe wabunifu zaidi ili kutoa mchango katika maendeleo ya Taifa na ustawi wa nchi kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunatatua kero zinazowakabili wananchi," Dk. Ndumbaro alisisitiza.

Katibu Mkuu huyo pia alitoa wito kwa wakuu wa utumishi wa umma hususani walio katika halmashauri na taasisi zenye matawi, kuwatembelea watumishi wanaowasimamia kwenye maeneo yao ya kazi ili wabaini kero zinazowakabili na kuzitatua ili kuondoa shida ya watumishi kusafiri umbali mrefu kwenda makao makuu kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi kero zao.

"Mkiwafuata katika vituo vyao vya kazi, mtawasaidia kuwapunguzia gharama za kusafiri kwenda makao makuu ya wilaya, mkoa au makao makuu ya nchi kwa ajili ya kutatua changamoto zao kwani nyie viongozi mkiwatembelea serikali ndiyo itawagharamia," alifafanua.

Rais Samia tangu aingie madarakani Machi 19 mwaka jana, amekuwa mstari wa mbele kuboresha stahiki za watumishi wa umma nchini ili kuwajengea ari na morali ya kutoa huduma bora kwa wananchi na hatimaye wananchi wajivunie uwapo wa serikali yao.



Mke wa Rais wa Zimbabwe, Dkt. Amai Auxillia Mnangagwa, akifungua rasmi Kongamano la Tembo wa Afrika lililofanyika kwenye Hifadhi ya Hwange nchini Zimbabwe. Kulia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja. **PICHA: HAPPY SHAYO**

# BRELA yatoa sababu kufuta kampuni 5,600

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umetangaza kusudio la kuanza kuzifutia usajili jumla ya kampuni za kibiashara 5,676 zilizoshindwa kukidhi vigezo vya kisheria.

Kwa mujibu wa wakala huo, uamuzi huo unachukuliwa kwa kuzingatia takwa la kisheria la kampuni kuwasilisha taarifa za mwaka kwa kampuni zilizosajiliwa nchini au mizania ya mwaka kwa kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi kwa zaidi ya miaka 15.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari, akisema ufutaji wa usajili wa kampuni hizo utafanyika kwa awamu. Alisema awamu ya kwanza itajumuisha kampuni 5,676. Kati yake, kampuni 5,284 zimesajiliwa nchini na zingine 392 ni zilizosajiliwa nchi za nje na kupata hati ya utambuzi. Nyaisa alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa vifungu vya 400 na 441 vya sheria ya kampuni ambayo inampa mamlaka msajili wa kampuni kufuta kampuni ambayo haijaonyesha kuendelea kufanya biashara au kuendelea kushikilia majina kinyume cha sheria.

"Hali hii inawazuia watu wengi wenye uhitaji wa majina hayo kuyatumia lakini pia inapunguza Pato la Taifa na kuisababishi hasara kwa serikali.

"Faida ya zoezi ni kuhakikisha daftari la usajili wa kampuni linakuwa na taarifa sahihi za kampuni, daftari kubaki na kampuni ambazo ni hai, kuutaarifa umma kuhusu uhai wa kampuni na kuwakumbusha wamiliki wa kampuni juu la kujumu lao la kuwasilisha taarifa kwa msajili kila mwaka," alifafanua.

Alikumbusha kuwa kifungu cha 128 cha Sheria ya Kampuni, Sura 212, kinazitaka kampuni zilizosajiliwa nchini kuwasilisha taarifa za mwaka, akifafanua kuwa kutowasilisha taarifa hizo kunatoa tafsiri kuwa kampuni hizo hazifanyi biashara kulingana na lengo la kuanzishwa kwake.

Alisema kifungu cha 438 cha sheria hiyo kinazitaka kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi ambazo zinafanya biashara nchini, kuwasilisha mizania ya mwaka, kinyume cha hapo inatafsiriwa kuwa kampuni hizo hazina tawi nchini.

Nyaisa alitoa rai kwa kampuni zilizosajiliwa chini ya sheria hiyo kutekeleza matakwa ya sheria kwa kuwasilisha taarifa za mwaka (Annual Returns) ili kuepuka kufutwa kwenye datfari la kampuni kwa kuwa ufutaji wa kampuni zenye dosari tajwa hapo juu, ni endelevu. "Kutokana na vifungu tajwa hapo juu, msajili wa kampuni anatoa notisi ya siku 30 kuanzia Mei 30, mwaka huu ili kampuni tajwa zithibitishe kwamba bado zinafanya biashara. Kampuni ambazo hazitatekeleza matakwa ya taarifa hii zitaondolewa katika daftari la kampuni zilizosajiliwa nchini," alionya na kubanisha kuwa orodha kamili ya kampuni hizo inapatikana kwenye tovuti rasmi ya BRELA.

Nyaisa aliendelea kufafanua, akisema: "Endapo kampuni husika, wanahisa au wadeni wa kampuni, zikiwamo taasisi za kifedha na watumishi wa kampuni wanaamini kwamba kampuni iliyoko kwenye orodha hii inafanya biashara na kwamba inapaswa kubaki kwenye daftari la kampuni zote, watoe taarifa kwa msajili wa kampuni kupitia anwani ya Posta."

# Chongolo ashtukia mchezo mchafu uchaguzi wa CCM

**Na Maulid Mmbaga,** SHINYANGA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amepiga marufuku katibu wa ngazi husika anayegombea, kushiriki katika mchakato wa utoaji fomu kwa wagombea wengine ili kuepusha udanganyifu na ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi ndani ya chama hicho.

Aliagiza hayo jana mkoani Shinyanga alipowasalimia wananchi baada ya kuwasili katika makao makuu ya chama hicho mkoani hapa, akiagiza uongozi wa eneo husika kutafuta mtu mwingine wa kusimamia suala hilo.

Chongolo alisema chama hicho kina taratibu zake, katiba, kanuni na miongozo iliyoandikwa kwa weledi, hivyo hawawezi kuwa na mtu anayeshindana na wenzake ilhali yeye yuko ndani.

"Yaani mimi ni mchezaji nakwenda na mpira nimeushika kwapani mpaka karibu na goli, si nitafunga tu! Hiyo siyo sawa, ninatoa agizo pale ambapo kuna kiongozi wa ngazi husika anagombea, kiongozi huyo atakaa pembeni, asishiriki vikao vya uamuzi hapo ili awatendee haki wenzake na wenzake wamtendee haki yeye.

"Chagueni mtu mwingine kutoka pembeni aingie ndani akae pale, au kama kwenye kamati ya siasa wote wanagombea pandisheni kwenye halmashauri kuu mshushe mtu mmoja mzuri, kama ni katibu wa vijana ashuke asimamie uchaguzi ili kuwatendea haki watu wote," aliagiza.

Alisema tatizo lililopo ni pamoja na baadhi ya watu wanaopewa dhamana katika maeneo kutotenda haki, huku akisisitiza kuwa ni marufuku mtu yeyote kuonewa kwa shutuma, majungu, uongo na kusingiziwa.


"Lazima tutende haki, wakati wote wa miaka mitano iliyopita toka 2017 mtu anafanya kazi, yupo, hana tatizo lolote kwenye kikao cha maadili, kuulizwa na cha kuhojiwa haitwi, imefika wakati wa uchaguzi kikao asubuhi, mchana, jioni huyu mbaya, mrefu, mfupi, mnene, anakuhusu nini?

"Kwa nini hukumwita kipindi chote unasubiri wakati wa uchaguzi? Huo ni ujanja ujanja wa kukatana majina, hiyo siyo sawa, tumekuja na lazima tuseme ukweli na niwapongeze kwa kusimamia vizuri uchaguzi wa shina nchi nzima na kwa Mkoa wa Shinyanga," alisema.

Vilevile, aliwataka viongozi wa chama hicho kuacha kufanya vitu ambavyo havina ulazima kwa wakati husika, akifafanua kuwa kiongozi anayefanya kampeni muda ambao siyo maalum kwa kazi hiyo, hatoshi kuwa kiongozi.

Chongolo alianza ziara jana mkoani Shinyanga ikiwa ni mara yake ya kwanza kufika mkoani hapa tangu ashike wadhifa huo. Alitaja sababu tatu za kuzuru mkoani hapa kuwa ni kuwasalimia wanachama wa chama hicho na wananchi, kukagua uhai wa chama na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ndani yake ina ahadi za utekelezaji kwa ajili ya wananchi.

Akiwa mkoani hapa jana, kiongozi huyo wa CCM alikagua baadhi ya vituo vya afya ana kubaini kuwapo uhaba wa watumishi wa kada ya afya na kuahidi kulifikisha suala hilo serikalini ili kibali cha ajira za watumishi kilichotolewa hivi karibuni, kiwanufaishe wananchi wa Shinyanga pia.




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka, akimpongeza Mhadhiri wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dk. Aldo Kitalika baada ya kumkabidhi mfano wa Hundi ya Sh. milioni 20 iliyotolewa na Benki ya NMB kwa mshindi wa jumla katika Wiki ya Maonyesho ya 7 ya Utafiti na Ubunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wa pili kushoto ni Meneja Utafiti, Masoko na Ubunifu wa NMB, Prochest Kachenje. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabula awatuliza wabunge utendaji kamati mawaziri 8

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAKATI wabunge wakilalamikia mawaziri wanane waliokwenda kutatua migogoro ya ardhi, kutofika maeneo yenye migogoro, serikali imejibu kwa kuwataka wawaamini viongozi wao na wa ngazi za mikoa kwa kuwa hakuna utatuzi utakaofanyika bila kushirikisha wananchi.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akihitimisha hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Baadhi ya wabunge, wakichangia bajeti ya wizara hiyo juzi na jana, waliwalalamikia mawaziri hao wanane waliokwenda kutatua migogoro ya ardhi kuwa hawakufika maeneo yenye migogoro badala yake waliishia ofisini kwa wakuu wa mikoa husika.

Akijibu hoja hiyo, Waziri Mabula alisema ni moja hoja zilizopigiwa kelele na wabunge waliochangia bungeni, akifafanua:

"Kinachofanyika pamoja na mawaziri wanane kwenda katika ngazi ya mikoa, tukumbuke ile mikoa saba au minane ya mwanzo kamati ile ilikuwa inakwenda kwenye vijiji, inaongea na wananchi na baadaye inakuja inawaachia mkoa kuendelea na ile shughuli na timu ya wataalamu inabaki.

"Ukihesabu vijiji hivyo kama ngazi ya kitaifa peke yake itakuwa inakwenda kwenye maeneo mengi, hiki tunachokipigia kelele cha migogoro kitachelewa kutatuliwa kwa sababu siyo rahisi ngazi ya kitaifa kwenda vijiji vyote na kumaliza, tunaachia mamlaka ya mkoa wanaofahamu maeneo yao, wanaoweza kuzungumza na watu ambapo sisi tumeshatoa maelekezo."

Waziri Mabula alisema kama serikali wanachofanya ni kuzitaka mamlaka zilizopo kwenye maeneo ambayo bado yanafanyiwa tathmini kuangalia uhalisia wa maeneo hayo wakisaidia na wataalamu wao ili yaachwe kama yalivyo wananchi waendelee kufanya shughuli zao au kuna haja ya kuwaondoa ili miradi iwe salama.

"Hii tathmini bado inaendelea mpaka sasa ninavyozungumza siwezi kukwambia nani na nani ataondoka pale mpaka ile tathmini ikamilike na wataalamu wapo.

"Niwaombe wabunge, fedha nyingi mnapitisha kwa ajili ya miradi ya kitaifa, tukiidhinisha fedha halafu tukataka kukwamisha mwisho wa siku tutapoteza nguvu ya umma, na fedha ya serikali kwa kukwamisha miradi ambayo tunajua ni vielelezo kwa Taifa," alisema.

Waziri Mabula aliwaomba wabunge katika vijiji ambavyo tathmini inaendelea wawaamini viongozi wa ngazi za mikoa na serikali kwa sababu hakuna utatuzi utakaofanyika bila kushirikisha wananchi.

"Wananchi watashirikishwa sehemu zote na maelekezo ya serikali ndivyo yalivyo. Kwa hiyo, tutakuwa tunakwenda kutoa maelekezo, ninaomba hili lieleweke kwa sababu limechukua kidogo wazungumzaji wanaotoka maeneo hayo wamezungumza sana ikiwamo GN28 ambayo ni kati ya yale yanayokwenda kufanyiwa kazi kwenye ukanda huo," alisema.

Aliwaeleza wabunge kuwa wanastahili kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu vijiji 975 angekuwa ni Rais ambaye siyo msikivu, asingeridhia vijiji 920 kurasimishwa.

Alisema katika utatuzi huo maelekezo ndani ya serikali ni kwamba lazima waangalie vijiji ambavyo havina athari virasimishwe.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete, alisema kwa migogoro ambayo imetajwa na wabunge ukiwamo wa Efatha kule Rukwa, maelekezo ya wizara yameshatolewa namna ya kuitatua.

**MICHANGO YA WABUNGE**

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, akichangia juzi, alisema mawaziri hao hawakwenda kwenye maeneo yenye migogoro kuwasikiliza wananchi, bali waliishia kujifungia ofisini kwa wakuu wa mikoa husika.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, alisema yupo kwenye kamati inayohusiana na ardhi na mwenzao aliomba mwongozo.

"Kamati hii ya mawaziri nane ilikuwa haijawahi kutoa taarifa, tulivyoomba walitupa taarifa kidogo. Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona badala ya kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi tumekwenda kufukua moto ambao sijui huko mbele ardhi itakwenda kuwa namna gani," alisema.

Mbunge huyo alisema mawaziri wanane wanaokwenda kwenye majimbo na mikoa waonane na wananchi siyo kuishia kwenye ofisi za wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya.

Alisema wanakwenda kwa wananchi wanaopokuta sehemu imetulia lakini wakikuta moto unafuka hawaendi wanaishia ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya.

"Inawezekana hii kamati ya mawaziri wanane ikawa ni mwiba kwa wananchi kuliko kawaida ninakuomba Mheshimiwa waziri mkienda kule, mkawaone wanachi, waambieni mnachokwenda kukifanya, zile kamati ndogo mnazoziacha kule chini ndiyo mwiba mchungu kwa wananchi," alitoa angalizo.

**MPANGO MIJI**

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema endapo nchi ikipimwa, migogoro itapungua na kuitaka serikali iongeze fedha kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ili nchi ipimwe na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutambuliwa na taasisi za fedha pindi wanapotafuta fursa za mikopo.

Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, Halima Mdee, alishikilia shilingi (mshahara wa waziri), akisema Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2021/22-2024/25 pamoja na mambo mengine umeelekeza ndani ya miaka mitano wawe wamepanga vijiji 6,160 kati ya 12,312 ambapo mpaka sasa asilimia 75 ya ardhi mijini haijapangwa.

Mbunge huyo alisema kuna haja ya tume kuongezwa fedha ili ikafanye kazi yake na mwaka ujao wabunge wasiambiwe "mawaziri wamekwenda kuzurura kutatua migogoro", bali tume hiyo imepewa fedha na kuongezwa rasilimaliwatu na kushirikiana na halmashauri kupanga.

Akifafanua suala hilo, Waziri Mabula alisema anachokisema mbunge huyo ni sahihi na katika hilo serikali inachokifanya pamoja na kwamba tume hiyo haijapewa fedha za kutosha, ipo mikopo iliyopata Dola milioni 150 ambazo zinakwenda kugusa wilaya 40, zitawekewa mpango wa matumizi bora wa ardhi na kufikia maeneo 50 kwa mwaka.

Pia alisema wamezungumza na Wizara ya Fedha na Mipango kuona ni namna kasi itaongezeka na kufikia lengo la maeneo 6,160, kauli ambayo ilimafanya mbunge huyo kuendelea kushikilia shilingi na kutoa hoja ambayo iliungwa mkono wa wabunge na mwishoni mwa mjadala Mdee alisema kwa kuwa ameamua kuwa 'chawa wa waziri'.

Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, alisema migogoro ya ardhi maeneo mbalimbali nchini, Kinondoni ikiwa ni kinara, inasababishwa na baadhi ya viongozi wa serikali wasio waaminifu ambao badala ya kutatua matatizo wanachochea na kuwachonganisha na serikali.

Spika wa Bunge, Tulia Ackson akizungumza baada ya hoja hiyo kupitishwa na Bunge, aliitaka serikali kufanyia kazi michango ya wabunge iliyotolewa.



Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto (kushoto), akikabidhi hati ya makubaliano kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Cecilia Mwambalaswa, baada ya kutia saini makubaliano ya kukabidhi kiwanda kwa shirika hilo kwenye hafla ya kukabidhi viwanda 10 vilivyobinafsishwa na kurejeshwa serikalini kwa taasisi tatu iliyofanyika Dar es Salaam jana. NDC imepewa kuendeleza kiwanda cha vipuri Mang'ula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viwanda 10 vilivyotelekezwa vyakabidhiwa ili kuendelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekabidhi kwa taasisi nne viwanda 10 ambavyo wawekezaji walishindwa kuviendeleza kulingana na mikataba ya mauzo, hivyo malengo ya serikali ya kubinafsisha kutotimia.

Taasisi zilizokabidhiwa viwanda hivyo ni Mamlaka ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB).

Agosti, mwaka jana, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, wakati huo, alitangaza na kutoa maelekezo kuhusiana na viwanda 20 vilivyorejeshwa serikalini na kusema viwanda 10 vihamishiwe katika taasisi za umma na viwanda 10 vitafutiwe wawekezaji kwa njia ya zabuni.

Akikabidhi viwanda hivyo jana jijini Dar es Salaam, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, aliwapa wakuu wa taasisi hizo wiki tatu kuhakikisha wanawasilisha mpango kazi ambao utafuatiliwa na ofisi yake.

"Ingawa leo (jana) nawakabidhi viwanda hivyo, mnatakiwa kuwasilisha mipango mikakati yenu ya kuendeleza viwanda hivi ifikapo Juni 20, mwaka huu," alisema Benedicto na kuongeza kuwa mipango watakayowasilisha ndiyo itatumika na Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya ufuatiliaji na tathmini juu ya utekelezaji wake.

Viwanda 10 ambavyo vimeelekezwa kuhamishiwa katika taasisi hizo ni TPL Shinyanga Meat Plant ambacho ni cha nyama, Mafuta Ilulu (Lindi), kiwanda cha kubangua korosho cha Nachingwea (Lindi), Mkata Sawmill Limited na Sikh Sawmill Limited (Tanga), Kiwanda cha Chuma Dar es Salaam na Mbeya Ceramic Ltd. Vingine ni Mang'ula Mechanical & Machine Tools (Morogoro), Mwanza Tanneries (Mwanza) na TPL Mbeya.

"Kati ya viwanda hivyo, Kiwanda cha Mang'ula Mechanical & Machine Tools kitahamishiwa NDC, Kiwanda cha Mbeya Ceramic kinakwenda SIDO na viwanda vinane vilivyobaki vinahamishiwa EPZA," alisema Benedicto.

Aliwataka viongozi wa taasisi hizo kuhakikisha wanatimiza malengo ya uwekezaji yakiwamo kuongeza uzalishaji, mapato kwa serikali, ajira, kuingiza teknolojia mpya katika sekta ya viwanda na uzalishaji na hatimaye kupunguza umasikini nchini.

Viwanda vilivyokabidhiwa EPZA ni TPL Shinyanga Meat Plant, Mafuta Ilulu, Nachingwea Cashewnut, Mkata Sawmill Limited, Sikh Sawmill Limited, National Steel Corporation na TPL Mbeya.

Aidha, Benedicto alisema Kiwanda cha Mwanza Tanneries, Msajili atakabidhi viwanja vitatu (Na. 2,4, na 5) kati ya vitano vilivyopo kwenye eneo hilo.

"Eneo lililobaki linasubiri maelekezo kutoka kwa mamlaka kabla ya kukabidhiwa rasmi kwa kuwa kulikuwa na maelekezo mengine ambayo yalitakiwa kukamilishwa kabla ya kufanya makabidhiano rasmi na EPZA" alisema.

Kuhusu Kiwanda cha TPL Mbeya ambacho kina eneo la Kiwanda (Plot Na. 760) na eneo la malishio ya wanyama (Nsalala Ground - Plot Na. 761), Msajili alisema atakabidhi eneo la Kiwanda tu huku akiendelea kusubiri maelekezo ya Serikali kuhusu Plot Na. 761. Kwa upande wa Kiwanda cha Chuma, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikabidhi eneo lililoko barabara ya Saza - Chang'ombe huku Bodi ya Mazao Mchanganyiko ikikabidhiwa kinu cha kukoboa mpunga kilichoko Kyela kwa ajili ya shughuli za ukoboaji. Pia ilikabidhiwa ghala la mazao wilayani Kiteto.

Awali, Mkurugenzi wa Ubinafsishaji katika Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mohamed Nyasama, alisema taasisi hizo zimeaminiwa na serikali, hivyo hazina budi kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza yale ambayo serikali inayatarajia katika kuimarisha uchumi wa nchi, lakini pia kusaidia ukuzaji wa ajira na kadhalika.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa taasisi zilizokabidhiwa viwanda hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alimshukuru Msajili wa Hazina kwa kuwaamini na kuwapa jukumu la kufufua na kuendeleza viwanja ili viweze kuleta tija kwa taifa.

"Nchi inahitaji wawekezaji. Ndiyo maana hata Rais wa nchi anazunguka huku na huko kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu kiuchumi. Tunajiona tuna deni kubwa kwa serikalini lakini kwa tunaamini kwa juhudi za pamoja, tutahakikisha kazi hii inafanyika na kuweza kutimiza malengo ya serikali katika uwekezaji nchini," alisema Itembe.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, Dk Anselm Moshi, alisema wanashukuru kwa fursa na kwamba wanakwenda kutekeleza maagizo waliyopewa huku akiahidi nchi kuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha.

# Jela miaka 20 kwa kuzini na bintiye

**Na Samson Chacha**, TARIME

MKAZI wa Mtaa wa Kebikiri Rebu, Kata ya Turwa, Tarime mkoani Mara, Daniel Mgohi (53) amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela baada ya kupatikana na hatia ya kuzini na binti yake wa kumzaa.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Yohana Myombo huku akibainisha kuwa anatiwa hatiani kutokana na ushahidi uliotolewa dhidi yake ambao haukuacha chembe yoyote ya shaka.

"Kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapa na upande wa mashitaka bila ya kuacha shaka yoyote, mtuhumiwa una hatia kutokana na kitendo ulichokifanya cha unyama cha kuzini na binti yako. Kwa hiyo ninakuhukumu kwenda jela miaka 20 ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama yako," alisema.

Awali, mwendesha mashitaka Mrakibu wa Polisi (SP) Esther Komba, alidai kuwa mtuhumiwa Mwita ambaye ni baba wa binti (jina linahifadhiwa) alifanya kitendo hicho usiku wa Desemba 21, 2021 nyumbani kwake.

Baada ya kufanya hivyo, Komba lidai kuwa binti huyo alilalamika na kutoa taarifa kwa mama yake na ndugu zake kuhusiana na kitendo hicho cha ukatili.

Komba alidai kuwa baada ya kuripoti tukio hilo, mama yake na ndugu zake walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi Tarime na kufungua jalada na kupewa fomu namba tatu ya polisi (PF 3) kwenda kufanyiwa uchunguzi Hospitali ya Wilaya.

Alidai kuwa ripoti ya uchunguzi wa kitabibu ilibainisha mtoto huyo kufanyiwa vitendo hivyo kwa kuzini na baba yake na mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Upande wa mashitaka ulipeleka mashahidi wanne akiwamo binti aliyefanyiwa kitendo hicho, nyaraka za hospitali, mganga aliyemfanyia uchunguzi na kuonyesha kufanyiwa vitendo hivyo.

Mshtakiwa hakuwa na shahidi mwingine wa kumuunga mkono mbali na kujitetea huku akidai kesi hiyo ilitengenezwa na ndugu zake ambao wana chuki naye kwa muda mrefu.

Katika kesi nyingine, amemuhukumu Mkazi wa Kijiji cha Kinesi wilayani Rorya, Chacha Kinemo, miaka mitatu jela na kutakiwa kulipa faini ya Sh. milioni mbili.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Myombo baada ya Kinemo kupatikana na hatia ya kummwagia mdogo wake petroli mikononi na kumchoma moto kwa kiberiti na kumsababishia ulemavu wa kudumu.

Kinemo alidaiwa alimfanyia unyama huo mdogo wake kwa madai ya kumwibia Sh. 185,000 jambo ambalo mdogo wake huyo alipinga kufanya hivyo.

HABARI KITAIFA

# Wizara yahadharisha ukosefu miundombinu rafiki kwa hedhi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, amesema kukosekana kwa miundombinu rafiki kwa wasichana au wanawake wakati wa hedhi, kunaweza kusababisha kupata maambukizi katika njia ya mkojo na hata kukumbwa na maradhi ambayo yanaweza kuwafanya kuwa wagumba.

Prof. Makubi alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari na maofisa wa afya kutoka wilaya zote za mkoa wa Tabora katika mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Mtemi Isike, Mwanakiyungi mjini hapa.

Alisema kitendo cha hedhi salama hakipewi nafasi kubwa kutoka kwa jamii, hivyo wanawake wanashindwa kupata watoto na kwamba kuna baadhi ya jamii zina imani potofu kiasi cha kuwanyanyapaa wanawake.

"Jamii nyingi zinahusisha hedhi na uchafu au najisi. Hali kadhalika, maumivu ya tumbo wakati wa hedhi huhisiwa kuwa msichana au mwanamke ametoa mimba au amejamiiana na mume wa mtu mwingine au anadanganya," alisema Prof. Makubi

Alisema wanawake au wasichana wengi huwa wanapata changamoto ya kutomudu gharama za taulo za kike, kupata maji salama na vyoo bora.

Kutokana na hali hiyo, alisema jamii inapaswa kutambua kuwa hedhi salama ni afya na ni baraka za uumbaji wa Mwenyezi Mungu.

Prof. Makubi alisema wizara itaendelea kutoa elimu ya hedhi salama kwa jamii kwa lengo la kuhamasisha, kuvunja ukimya na kuachana na mila na desturi potofu kuhusu hedhi.

Pia alisema watahakikisha Sera ya Afya inaliweka jambo la hedhi salama kuwa moja ya vipaumbele vyake ili kutunza heshima na utu wa mwanamke na kumpa nafasi ya kuleta maendeleo katika jamii.

Hedhi Salama ni msichana au mwanamke anapokuwa katika siku zake na anatakiwa kuwa katika mazingira salama na kupata huduma zote muhimu ikiwamo miundombinu ya vyoo vyenye usiri, maji safi, taulo za kike au vifaa salama vya kujisitiri pamoja na utupaji salama wa vifaa au taulo za kike zilizotumika.

# Kortini madai ya kukutwa na meno ya tembo ya milioni 176/-

**Na Grace Gurisha**

WAKAZI wawili wa Dar es Salaam, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashitaka ya kukutwa na vipande 19 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh milioni 175.8.

Washitakiwa hao ni Fadhil Saidi (44) ,mkulima na mkazi wa Kiwalani na Daniel Ndunguru (35) mjasiriamali na Mkazi wa Tandika.

Akisoma mashitaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate, Wakili wa Serikali Yusuph Aboud alidai kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo Mei 3, mwaka huu, maeneo ya Ukonga Sabasaba, Dar es Salaam.



Aboud alidai kuwa washitakiwa kwa pamoja walikutwa na vipande 19 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Dola za Marekani 750,000 (sawa na Sh. 175,875,000) bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Washitakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote na upande wa mashitaka ulidai upelelezi wa shauri hilo unaendelea, hivyo aliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Steven Mbwana, alidai sheria mpya ya uhujumu uchumi inaipa mahakama mamlaka ya kutoa dhamana iwapo thamani ya fedha hazijazidi Sh. milioni 300, hivyo aliomba washitakiwa wapatiwe dhamana.

Hakimu Kabate alimtaka kila mshitakiwa kuwa na fedha taslimu au kuwasilisha hati ya mali yenye thamani ya Sh 43,968,750.

Pia aliwataka kuwa na wadhamini wawili kila mmoja, watakaotia saini bondi ya Sh. milioni 20 sambamba na kuwa na utambulisho kutoka taasisi au sehemu anayofanyia kazi.

Washitakiwa hao pia walitakiwa kuwasilisha mahakamani hapo hati zao za kusafiria na kwamba hawataruhusiwa kutoka nje ya mamlaka hiyo bila kibali cha mahakama.

Washitakiwa walirudishwa rumande hadi Juni 9, mwaka huu, baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**Kiambatisho III**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUITWA KUANZA MAFUNZO YA STADI ZA KAZI KATIKA FANI MBALIMBALI KWA NJIA YA UANAGENZI**

Itakumbukwa kuwa tarehe **31 Machi, 2022 Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (OWM-KVAU)** ilitangaza fursa za mafunzo ambayo yatatolewa katika taasisi za mafunzo zilizotangazwa kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara. Ofisi ya Waziri Mkuu inapenda kuutaarifu umma kuwa vijana **7,760** wamechaguliwa kujiunga na mafunzo katika vyuo **62** nchini. Majina ya vijana waliochaguliwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo za vyuo husika na katika tovuti ya www.kazi.go.tz. Vijana waliochaguliwa wanatakiwa kuripoti kwenye vyuo hivyo kwa ajili ya kujisajili kuanzia tarehe **30 Mei, 2022** Mafunzo yataanza rasmi tarehe **6 Juni, 2022**. Mikoa na vyuo husika ni kama ifuatavyo: -

| MKOA | JINA LA CHUO | |
|---|---|---|
| ARUSHA | 1. | ARUSHA - DON BOSCO KII - TECH |
| | 2. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MTO WA MBU |
| | 3. | CHUO CHA HOTEL NA UTALII VETA NJIRO |
| DAR ES SALAAM | 4. | DON BOSCO OYSTERBAY VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 5. | CHUO CHA UFUNDI YOMBO KWA WATU WENYE ULEMAVU |
| | 6. | CHUO CHA VETA DAR ES SALAAM |
| | 7. | VETA KIPAWA |
| DODOMA | 8. | DON BOSCO TECHNICAL INSTITUTE (DODOMA) |
| | 9. | CHUO CHA VETA DODOMA |
| GEITA | 10. | GEITA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| IRINGA | 11. | IRINGA - DON BOSCO YOUTH TRAINING CENTRE |
| | 12. | CHUO CHA VETA IRINGA |
| | 13. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI ILULA, FDC |
| KAGERA | 14. | KAGERA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 15. | KARAGWE DVTC |
| KATAVI | 16. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MSAGINYA, FDC |
| | 17. | MPANDA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| KIGOMA | 18. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KASULU, FDC |
| | 19. | CHUO CHA VETA KIGOMA |
| | 20. | NYAMIDAHO DVTC |
| KILIMANJARO | 21. | MARANGU SCHOOL OF TOURISM AND VOCATIONAL TRAINING |
| | 22. | CHUO CHA VETA MOSHI |
| LINDI | 23. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KILWA MASOKO, FDC |
| | 24. | CHUO CHA VETA LINDI |
| | 25. | RUANGWA DVTC |
| MANYARA | 26. | MANYARA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| MARA | 27. | MARA - ST. ANTHONY VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 28. | LAKE VICTORIA DISABILITY VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 29. | MARA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| MBEYA | 30. | CHUO CHA UFUNDI CHA MAGEREZA RUANDA |
| | 31. | BUSOKELO VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 32. | CHUO CHA VETA MBEYA |
| MOROGORO | 33. | CHUO CHA VETA KIHONDA |
| | 34. | MIKUMI VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| MTWARA | 35. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MASASI (MASASI FDC) |
| | 36. | MTWARA RVTC |
| MWANZA | 37. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SENGEREMA, FDC |
| | 38. | CHUO CHA VETA MWANZA |
| NJOMBE | 39. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NJOMBE, FDC |
| | 40. | MAKETE DVTC |
| PWANI | 41. | CHUO CHA VETA PWANI |
| RUKWA | 42. | MVIMWA VOCATIONAL TRANING CENTER |
| | 43. | CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (RUKWA KAMPASI) |
| | 44. | LAELA AGRICULTURAL VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| RUVUMA | 45. | PERAMIHO VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 46. | CHUO CHA VETA SONGEA |
| | 47. | MPAPA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 48. | CHIPOLE VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| SHINYANGA | 49. | SHINYANGA - OLA SISTERS (BUGISI VTC) |
| | 50. | SHINYANGA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| SIMIYU | 51. | CHUO CHA UFUNDI STADI BINZA (BINZA VTC) |
| | 52. | KANADI DVTC |
| SINGIDA | 53. | CHUO CHA UFUNDI NA MAREKEBISHO KWA WATU WENYE ULEMAVU SABASABA |
| | 54. | SINGIDA VOCATIONAL TRAINING CENTER |
| | 55. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SINGIDA, FDC |
| SONGWE | 56. | DAR ES SALAAM INSTITUTE OF TECHNOLOGY MYUNGA |
| | 57. | ILEJE DVTC |
| TABORA | 58. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NZEGA, FDC |
| | 59. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI URAMBO, FDC |
| | 60. | CHUO CHA VETA TABORA |
| TANGA | 61. | CHUO CHA VETA TANGA |
| | 62. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI HANDENI, FDC |

**IMETOLEWA NA:**
**KATIBU MKUU**

216877402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga, Simba tunatarajia mchezo wa kiwango bora

**MIAMBA** ya soka Tanzania, Yanga na Simba leo Jumamosi inashuka kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Jijini Mwanza kuwania kutinga fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam maarufu kama FA.

Mchezo huo wa hatua ya nusu fainali unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kutokana na timu zote mbili kuhitaji kutinga fainali na hatimaye kulitwaa taji hilo.

Timu hizo zinaingia kwenye mchezo huo, wakati Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni kabla ya kufungwa rasmi kwa pazia la msimu huu.

Nipashe tukiwa kama wadau wakuu wa michezo hapa Tanzania, tunaamini mchezo huo utakuwa wa kiwango bora na cha juu kwa timu zote mbili hasa ikizingatiwa kwamba, hizo ndio kama baba na mama wa soka la hapa nchini.

Tunaamini timu zote zimejipanga vizuri kuelekea mchezo huo na kwa namna yoyote utakuwa na burudani nzuri na kutosha kwa mashabiki wao.

Yanga itaingia kwenye mchezo huo ikiwategemea zaidi wachezaji wake kama kipa Djigui Diarra safu yake ya ulinzi chini ya nahodha Bakari Mwamnyeto, Yannick Bangala, Djuma Shabani na Kibwana Shomari.

Wakati katika eneo la kiungo atakuwepo Khalid Aucho, Salum Abubakary 'Sure Boy' na Feisal Salum 'Fei Toto' huku Fiston Mayele akitarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji sambamba na Jesus Moloko.

Kwa upande wa Simba kuna shaka ya uwepo wa golikipa wao namba moja, Aishi Manula na huenda ikampa nafasi Beno Kakolanya ambaye ni kipa wa zamani wa Yanga, kuanza au kuingia kwenye mchezo huo huku Hennock Inonga na Joash Onyango wakitarajiwa kuanza kwenye beki ya kati.

Sehemu ya kiungo ya Simba huenda ikaanza na Taddeo Lwanga, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute na viungo wa pembeni akawatumia Pape Sakho, Larry Bwalya na kwenye eneo la ushambuliaji akaanza na nahodha John Bocco na Kibu Denis.

Kutokana na uimara wa vikosi vyote vya timu hizo, sisi tuna imani kubwa utakuwa mchezo wa kutumia mbinu, akili na ubunifu wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba, mmoja anaibuka na ushindi.

Uzuri wa mchezo wa leo ni kwamba, kwa namna yoyote lazima mshindi apatikane, kwani hapa inatafutwa timu itakayotinga fainali.


Hivyo, tunaamini kabisa kwa jinsi makocha na mabenchi yao ya ufundi walivyojipanga, tunatarajia kutakuwa na burudani ya ina yake wakati dakika 90 au muda wa ziada au penalti zitakapomalizika.

Hatutarajii lawama za namna yoyote kwa kuwanyoshea kidole waamuzi au maofisa mara baada ya mchezo huo, kwani kila timu ilikuwa na nafasi ya kujifua kabla ya kuingia kwenye mchezo huo na maana yake ni kwamba walikuwa wamejiandaa vya kutosha.

Mshindi wa mchezo wa leo atakutana kwenye fainali na mshindi kati ya Azam FC na Coastal Union ambao wao watakipiga kesho Jumapili kwenye uwanja wa Sheikh Amri Abeid kule jijini Arusha.

Hivyo basi, tunawatakia Yanga na Simba kila la heri katika mchezo huo ambao tunaamini utakuwa bora na wenye ushindani ambao matokeo yake yataamuliwa uwanjani kutokana na kiwango bora cha timu itakachokionesha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Marefa wachezeshe 'dabi' kwa haki, waaminike

Na Adam Fungamwango

**LEO** kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza kutakuwa na bonge la mechi, nusu fainali ya Kombe la FA ikizikutanisha timu hasimu za Simba na Yanga kutafuta timu itakayokwenda kucheza fainali ya michuano hiyo.

Bingwa wa michuano hiyo huiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), hivyo ukiliangalia pambano hili kwa makini ni kwamba hakuna timu yoyote kati ya hizo inayohitaji nafasi ya kucheza michuano hiyo zaidi tu ya kutaka ushindi na kombe lenyewe.

Ni kwa sababu timu zote mbili msimu ujao zina tiketi ya kwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo Simba na Yanga zinakwenda kucheza mechi hiyo zikiwa na malengo mengine kabisa.

Simba na Yanga zinacheza mechi hiyo, kila mmoja akitaka kushinda kwanza kabisa ni kwa sababu tu ya utani wao wa jadi wa miaka nenda rudi.

Simba inataka kushinda mechi hiyo na hatimaye kwenda fainali kushinda kombe hilo ili kujifariji isitoke kapa msimu huu, kwani inaelekea kuukosa Ubingwa wa Tanzania Bara.

Yanga inachotaka kwanza ni kuifunga Simba ili utani utimie, lakini pia kama itashinda na kwenda kuchukua ubingwa inataka kufanya hivyo ili kuwa kama watani zao hao ambao walikuwa wakitwaa Ngao ya Jamii, Ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA. Lakini pia 'kuibania' Simba ili msimu huu itoke patupu kama Simba ilivyoifanyia kwa misimu miwili iliyopita.

Hayo ndiyo malengo ya timu hizo na wala si kucheza mechi za kimataifa, kwani tayari zina tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Kamati ya Waamuzi imewatangaza Ahmed Aragija wa Manyara kuwa mwamuzi wa kati, mwamuzi msaidizi namba moja ni Frank Komba wa Dar es Salaam na msaidizi namba mbili ni Mohamed Mkono kutoka Tanga, huku mwamuzi wa akiba, akiwa tayari kwa lolote litakalotokea anaweza kuingia yeye anapuliza kipenga ni Elly Sasii wa Dar es Salaam.

Wote waliochaguliwa ni waamuzi wazuri sana, lakini kwenye nchi hii linapokuja suala la Simba na Yanga mambo hubadilika kabisa.

Mwamuzi anaweza kuwa mzuri na bora, lakini kwenye mechi hiyo akafanya vitu ambavyo kila mmoja akashangaa.

Inaonekana kama waamuzi wamekuwa wakichezesha kwa kuogopa mechi hizi. Na wanachoogopa ni lawama. Ndiyo maana wakati mwingine wanachezesha kwa kutaka kusawazisha mambo.

Anapofanya kosa mchezaji wa timu moja akashindwa kumpa kadi, basi wa timu nyingine akifanya ataogopa kufanya hivyo kwa sababu yule wa kwanza hakumpa.

Wakati mwingine kuna rafu za kadi za njano moja kwa moja, lakini wamekuwa hawatoi, mpaka huyo huyo acheze mara tatu za aina hiyo, ndiyo atapewa hiyo kadi.

Ifike wakati waamuzi waache woga, kama mtu kakwatuliwa ndani ya eneo la hatari, basi iwe penalti tu, na kama mchezaji kaushika kwa makusudi 'tuta' liwekwe tu hata kama matatu au manne, ili mradi iwe kweli kuna makosa.

Unaweza ukaona kabisa kuwa kuna timu haiko vizuri na inaelekea kufungwa, lakini utakuta baadhi ya waamuzi wanakuwa kama wao ndiyo wanaufanya mchezo uwe mgumu kwa timu iliyo kwenye nafasi nzuri ya kushinda.

Mimi nadhani kama mwamuzi anachezesha kwa kufuata sheria, mechi ya Simba na Yanga ni rahisi sana kuicheza kwa sababu mara nyingi wanacheza wanachezaji wanaojitambua, lakini kuna wakati waamuzi wataitia mechi ugumu wenyewe na wao kujiingiza kwenye lawama kwa sababu ya kutaka 'kubalansi'.

Acha timu iliyoelekea kufungwa ifungwe hata mabao sita, ili ijue makosa yake ikayatatue, ili mradi tu wawe wamechezesha kwa haki.

Binafsi ninawatakia mchezo mwema waamuzi wa mechi hiyo, lakini nawasihi waache woga wa maamuzi magumu kama ambavyo huwa tunaona kwenye mechi zilizopita.

Hili wasiliangalie sana, wao waangalie sheria na kanuni zinasema nini. Unapochezesha kwa haki, hata mashabiki wa timu iliyofungwa na kulalamika kwa jazba, baadaye watakuja kukuheshimu hasira zao zitakapokuwa zimepungua.

Lakini waamuzi wanapoinyonga timu, kwa ajili ya kuipa furaha timu moja, mashabiki wa timu nyingine wanakuwa hawana imani tena na mwamuzi huyo hata kama akiwachezesha vizuri vipi kwenye mechi zinazofuata. Waamuzi wachezeshe kwa haki mechi ya leo ili waendelee kuaminika.

## Serikali kuhuisha kiwanda Mang'ula

SERIKALI imeamua kukihuisha upya kiwanda cha Mang'ula Mechanical & Machine Tools Co. Ltd (MMMT) kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ili kiendelee kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa hapo awali.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nyasa (CCM), Mhandisi Stella Manyanya.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni kwa nini serikali isitoe rasilimali za kiwanda cha Mang'ula Mechanical and Machine Tools kilichoko Kilombero kwa taasisi za ufundi kama DIT na zingine ili kutumia.

Kigahe alisema ikiwa kutakuwa na haja ya kuzihusisha taasisi za ufundi, Serikali itafanya hivyo.

Alikiri kuwa NDC ina miradi mingi yenye matatizo lakini serikali imeanza kushughulikia hilo ambapo fedha zimepelekwa za kutosha za kuhuwisha Moshi machine tools.

"Aidha, tunaangalia nini kinahitajika kwa Mang'ula, tupo kwenye hatua za awali za utafiti wa nini kitafanyika," alisema.

Pia alisema kuhusu mitambo iliyokuwapo Mang'ula, inatakiwa kuhuishwa kwa kuwa mwekezaji wa awali aling'oa mitambo mingi na kuuza.

"Tutaanza upya lakini nia ya serikali ni kuhuwisha viwanda hivi na serikali imeweka mkazo na itatenga bajeti ili kuhakikisha kinarudi kwenye uhalisia wake wa awali,"alisema.

## Mradi wa maji sasa kukamilika Desemba

Bunge limeelezwa mradi wa maji wa Oldonyo Sambu wilayani Arumeru unatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliliambia bunge jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Lemburis, aliyetaka kujua lini serikali itakamilisha ahadi ya Rais ya kujenga mradi wa maji wa vijiji tisa vya kata za Oldonyo Sambu na Oldonyowas.

Akijibu swali hilo, Mahundi alisema serikali inatekeleza mradi wa maji wa Oldonyosambu kwa ajili ya kuhudumia vijiji hivyo vya kata za Oldonyo sambu na Oldonyowas na utekelezaji wa mradi huo unahusisha ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 47.8.

Pia alisema unahusisha ujenzi wa matanki matatu yenye ujazo wa lita 575,000, ujenzi wa vituo vitatu vya kuchotea maji na booster stations mbili.

# Mbunge ahoji sera elimu bila malipo

MBUNGE wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima, amehoji mpango wa serikali wa kukabiliana na uhaba wa walimu, madarasa, samani na miundombinu mingine inayochagizwa na utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo.

Akijibu swali hilo jana bungeni, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua kukabiliana na upungufu wa walimu katika Shule za Msingi na Sekondari nchini kwa kuajiri walimu.

Pia alisema kuwapanga kwenye maeneo yenye uhaba, kufanya msawazo wa walimu katika maeneo yasiyo na walimu wa kutosha.

"Serikali katika kukabiliana na changamoto ya miundombinu ya elimu inaendelea kujenga shule mpya, madarasa yenye samani ndani yake na kuboresha miundombinu chakavu kupitia bajeti ya serikali na miradi ya kuboresha elimu kama vile BOOST, SEQUIP, EP4R na GPE LANES II," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya, alihoji lini serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga shule mpya katika kata ya Makutupora jimboni humo ili kutekeleza ahadi yake.

"Kwa kuwa utoaji wa elimu ya awali kwa mkoa wa Singida bado ni hafifu, je, nini mpango wa serikali kuhakikisha kwamba tunaajiri walimu hususan maeneo ya vijiji ya Mkoa wa Singida?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, alisema ahadi ya serikali ya kujenga shule mpya ya sekondari katika kata ya Makutupora ipo pale pale kwa kuwa fedha zipo kwenye bajeti.

Hata hivyo, alisema katika ajira za walimu zilizotangazwa moja ya kigezo kilichozingatiwa ni kuajiri walimu wampya ambao wana shahada ya elimu ya awali na stashahada ambao watapelekwa kwenye shule zote nchini ili kusaidia elimu hiyo nchini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, George Mkuchika (kulia) akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (kushoto) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk Eliezer Feleshi (katikati) Bungeni Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakiukaji mikopo halmashauri kubanwa

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema inaandaa mpango kuvibana vikundi vinavyokopa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa Halmashauri ili kuhakikisha vinalipa kwa wakati.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Regina Qwaray, ambaye alihoji kama serikali haioni haja ya kuongeza kiwango cha mikopo ya vikundi vya watu watano inayotolewa na halmashauri kutoka Sh. milioni moja hadi tano.

Pia alihoji serikali inachukua hatua gani kwa vikundi ambavyo vinashindwa kurejesha mikopo ili vingine vipate.


"Je, serikali haioni kama kuna haja ya kufanya uchambuzi wa kina kabla ya kutoa mikopo kwenye vikundi hivyo?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema kumekuwapo na hatua zinazochukuliwa kwa wasiorejesha mikopo ikiwamo kuwafuata kuwaelimisha na wale wagumu wamekuwa wakipelekwa mahakamani.

Alisema kwa sasa wanatoa elimu kwa maofisa maendeleo ya jamii kufanya uchambuzi wa kina kwa wale wanaokopa ili mikopo hiyo iwe na tija.

Awali, alibainisha kuwa Kanuni ya Tisa ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya mwaka 2019 imeelekeza kwamba fedha za mikopo zitakazotolewa zitatumika kwa miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi.

Alisema mchakato huo utazingatia kuzingatia ushauri na mapendekezo ya Timu ya Menejimenti na Kamati ya Huduma za Mikopo, hivyo ni jukumu la kikundi husika kuomba mkopo kulingana na mahitaji ya mradi husika.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA




Balozi wa China nchini, Chen Mingjian (kulia), akibadilishana hati za makubaliano ya utekelezaji wa masuala ya utamaduni kati ya nchi hiyo na Tanzania na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, juzi Dar es Salaam. **PICHA: UBALOZI WA CHINA.**

# Tanzania na China zatiliana saini utekelezaji masuala ya utamaduni

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na China zimetiliana saini mpango wa utekelezaji wa makubaliano ya kiutamaduni kwa mwaka 2022 hadi 2025.

Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Tanzania, Mohamed Mchengerwa, walitia saini juzi jijini Dar es Salaam kwa niaba ya serikali hizo mbili.

Mpango huo wa utekelezaji unalenga kuimarisha mabadilishano na ushirikiano baina ya nchi hizo mbili katika nyanja za utamaduni, sanaa, utalii, uandishi wa habari, michezo na elimu na kuzidisha urafiki wa jadi kati ya China na Tanzania. Kwa mujibu wa taarifa ya habari iliyotolewa juzi na ubalozi wa China nchini, makubaliano hayo yana lengo la kukuza zaidi mabadilishano na ushirikiano katika nyanja za utamaduni, sanaa, vyombo vya habari, redio, filamu, televisheni, michezo na elimu, yaliyofikiwa Aprili, 1992.

Taarifa hiyo ya serikali hizo mbili inaeleza kuwasiliana kwa pande hizo ili kupitia upya mkataba huo kwa mujibu wa maendeleo katika maeneo husika na kutia saini mpango wa utekelezaji kila baada ya miaka minne mara kwa mara.

"Mpango wa utekelezaji wa 2022-2025 si tu utarahisisha ushirikiano katika nyanja za utamaduni, sanaa, elimu, vyombo vya habari na uchapishaji, redio, filamu, televisheni na michezo, kama ilivyojumuishwa katika programu ya awali ya utekelezaji lakini pia itahusu utalii.

"Hiyo ni kwa sababu Wizara ya Utamaduni na Utawala wa Kitaifa wa Utalii wa China zilikuwa zimeunganishwa na kuwa wizara mpya iliyopewa jina la Wizara ya Utamaduni na Utalii katika urekebishaji wa kitaasisi wa 2018," ilisema taarifa hiyo.

Kupitia makubaliano hayo, imekubaliwa na pande zote mbili kuwa mabadilishano na ushirikiano katika nyanja ya utalii utaimarishwa na nchi hizo mbili zitahimiza ushiriki mpana zaidi katika kukuza utalii na kugawana bidhaa za kitamaduni na utalii.

Balozi Chen alisema China na Tanzania zinafurahia urafiki wa jadi na nchi hizo mbili zimekuwa zikishirikiana na kuratibu kwa karibu na kwa ufanisi katika sekta kama vile utamaduni, sanaa, redio, filamu, televisheni, elimu na sayansi na teknolojia.

Alisisitiza kuwa ushirikiano katika nyanja zilizotajwa, umekuwa na nafasi muhimu katika kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi hizo mbili na kuwezesha mawasiliano ya kirafiki kati ya mataifa hayo mawili.

Kutiwa saini kwa programu mpya ya utekelezaji, kunaashiria kuimarika kwa uhusiano wa kirafiki kati ya China na Tanzania, ambao unalazimika kuboresha kiwango cha mawasiliano kati ya watu na watu kati ya nchi hizo.

Waziri Mchengerwa alisema ushirikiano wa kitamaduni kati ya China na Tanzania unaleta manufaa mengi kwa Tanzania.

Alisema upande wa Tanzania unafuraha na unajivunia kushirikiana na China katika nyanja za utamaduni, sanaa na michezo, na Tanzania itafanya na kutekeleza mpango huo kwa nguvu na uhai.

Pia alisisitiza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amezindua filamu ya kitalii iitwayo "Royal Tour" ambayo itaidhihirisha Tanzania katika soko la utalii la kimataifa na kwamba Tanzania inatarajia kuimarisha zaidi ushirikiano na China katika sekta ya utalii, ikitarajia kuwa uzuri na uhai wa Tanzania utavutia marafiki zaidi wapenda amani na wakarimu kutoka kwa Asia.

Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilihudhuriwa pia na Mshauri wa Utamaduni wa Ubalozi wa China nchini Tanzania, Wang Siping.

# Wanafunzi 626 Ruangwa wapatiwa taulo za kike

**Na Sabato Kasika,** RUANGWA

WANAFUNZI 626 wa shule nne za sekondari Ruangwa mkoani Lindi, wamepata msaada wa taulo 1,878 za kike, ambazo zitawasitiri katika kipindi cha miezi mitatu ijayo wakati wa hedhi.

Shule zilizonufaika na msaada huo uliotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Victoria Foundation ni Hawa Mchopa iliyoko Kata ya Malolo, Mary Majaliwa (Nandagala), Lucas Maria na Mnacho, zote katika Kata ya Mnacho.

Akizungumza kabla ya kukabidhi taulo hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Victoria Foundation, Vicky Kamata, alisema wanafunzi hao wamefikiwa kupitia mradi wa kitaifa wa Binti Ng'ara Fikia Malengo'.

"Victoria Fundation inatekeleza mradi huu kwa ngazi ya kitaifa kwa sababu ni muhimu na unalenga kuwapa uhakika wanafunzi wa kike kufika shule na kusoma wakati wote huku wakijiamini," alisema Kamata.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mradi huo ulianza mkoani Simiyu na sasa umefika Ruangwa mkoani Lindi na kisha ataufikisha mkoani Mtwara ambako pia watagawa taulo hizo kwa mabinti wengi zaidi.

Mbali na taulo hizo kwa wanafunzi wa kike, wavulana wa shule hizo nao wamenufaika kwa mafunzo ya jinsi ya kujitambua na namna bora ya kutumia mitandao ya kijamii wanapokuwa ndani na nje ya shule.

Mratibu wa Programu wa Victoria Foundation, Steven Mruma, alisema mbali na kugawa taulo hizo, taasisi hiyo ilipata fursa ya kuendesha semina kwa wanafunzi wa shule hizo na mada zilitolewa na Zamaradi Mketema kwa wasichana huku Emmanuel Mathias akitoa kwa wavulana.

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, akizungumza katika ugawaji wa taulo hizo, alionyesha kufurahishwa na mradi huo na malengo yake kwa wasichana walioko shuleni na kushauri ufanyike nchi nzima.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, alipongeza shirika la Victoria Faoundion kwa kuchagua Ruangwa na kusema anatamani lirudi wilayani humo kuwakomboa mabinti.

# Waziri Jafo aanika mkakati kuokoa misitu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mikakati mbalimbali ya kuokoa mifumo ya ikolojia nchini kutokana na takribani hekta 469,420 za misitu kuharibiwa kila mwaka.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kitaifa itafanyika Dodoma na yataambatana na Wiki ya Mazingira.

Alisema kila mwaka hekta hizo za misitu zinapotea na kutokana na uharibifu huo, kumekuwapo mikakati ya kuokoa hali hiyo.

"Pamoja na kuwapo kwa uharibifu wa mazingira nchini, tusifu mikakati mbalimbali ya kila mwaka ya kuondoa hii mifumo ya ikolojia kwa mfano maelekezo ya serikali ya kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kwa lengo la kupanda miti milioni 276 maana yake tuna 'replace' misitu iliyoharibiwa," alisema.

Pia alisema wataalamu wa misitu wanasema wastani wa asilimia 62 ya miti inayopandwa inahimili kubaki.

"Kinachofanyika kama juhudi zitaendelea kuwa kubwa kiasi hiki, kutakuwa na mafanikio makubwa na katika wiki hii, Siku ya Mazingira ni mtambuka si kupanda miti peke yake," alisema. Alisema mbali na misitu kuharibiwa pia kuna tatizo la utupaji holela wa taka pamoja na uwapo wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Hali hii inaathiri maisha ya viumbe mbalimbali ikiwamo ya mifumo ikolojia ambapo hadi sasa imeisababishia nchi hasara ya takriban asilimia tano ya pato la taifa. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira yaendelee kuwa chachu ya kuongeza kasi ya uhamasishaji wa jamii kushiriki shughuli za kuhifadhi na kutunza mazingira nchini," alisema.

Waziri Jafo alisema kilele cha maadhimisho hayo kitatanguliwa na Wiki ya Mazingira inayoanza Mei 28 hadi Juni 4, mwaka huu na kutakuwa na shughuli mbalimbali za hifadhi na usafi wa mazingira katika jiji la Dodoma.

"Kutakuwa pia na maonyesho ya wadau ya shughuli mbalimbali za kuhifadhi mazingira yatakayoanza Juni Mosi hadi 5, mwaka huu, katika viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma na kwenye kilele, Rais Samia Suluhu Hassan atahutubia wadau wa mazingira na taifa kwa ujumla kupitia vyombo vya habari, sambamba na kuzindua Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira," alisema.

Mpango huo, alisema utakuwa nyenzo muhimu katika kutoa mwongozo wa kuandaa na kutekeleza miradi na programu za kuhifadhi mazingira nchini.



## Miche 200,000 miti kuzalishwa Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KUELEKEA maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 5, mwaka huu, wadau wa mazingira mkoa wa Dodoma wamepanga kuotesha zaidi ya miti 200,000 ambayo itasambazwa maeneo mbalimbali ili kuendeleza kampeni ya 'Dodoma ya Kijani'.

Mkurugenzi wa kikundi cha Chapa Kazi kinachojihusisha na uoteshaji miti na usambazaji, Daruweshi Saidi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wadau wa mazingira, wakiwamo waandishi wa habari kuelekea maadhimisho hayo yatakayofanyika kitaifa mkoani Dodoma.

Maadhimisho hayo yatakayoanza kesho ni pamoja na kuhamasisha elimu kwa wadau mbalimbali kupanda na kuilinda miti ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mazingira na kufanya usafi.

Alisema miche hiyo itakayooteshwa ni pamoja na maua, matunda na kivuli ambayo itasambazwa maeneo ya taasisi na watu binafsi na kwenye majengo ya ofisi za serikali.

"Pamoja na kufanya biashara ya kuuza miche, tutatumia nafasi hiyo ya maadhimisho ya mwaka huu kuhakikisha tunasambaza miche ya miti hiyo ili kupambana na kampeni hiyo ya Dodoma kuwa ya kijani," alisema.

Alisema mbali na kikundi cha Chapa Kazi kujihusisha kuuza na kusambaza miti, pia kimekuwa sehemu kubwa ya utoaji wa elimu kwa wadau wa mazingira na wanafunzi shuleni na kwenye vyuo vikuu vya elimu.

"Kikundi kimekuwa kikitoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kupenda mazingira ambayo yamekuwa sehemu kubwa ya kujiinua kiuchumi pamoja na afya," alisema.

Mdau wa mazingira, Julian Bruno alisema kuelekea maadhimisho hayo, wadau wamedhamiria kufanya kampeni ya kupanda miti kwenye mitaa ya barabara ili kuboresha jiji.

Kampeni hiyo itakayofahamika kama mtaa na miti itakayopandwa kando kando ya barabara, itashirikisha watu wote na itasaidia utunzaji wa mazingira.

# Mhagama awashia moto watumishi wazembe, wabadhirifu mali za umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema hatamwonea huruma mtumishi yeyote mzembe, mwizi na mbadhirifu wa mali ya umma, huku akiagiza maofisa rasilimali watu kuzingatia kanuni za maadili ya utumishi wa umma za mwaka 2005.

Mhagama aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa wakuu wa idara za utawala na rasilimali watu katika utumishi wa umma, uliofanyika jijini hapa.

"Utumishi wa umma unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za kushuka kwa uadilifu wa kazi katika utumishi wa umma," alisema.

"Ninapozungumzia uadilifu ninamaanisha masuala yote yanayohusu nidhamu, kushuka kwa weledi, ubadhirifu, kutozingatiwa kwa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi na menejimenti ya rasilimali watu," alisema.

Alisema hali hiyo inajidhihirisha kuwapo na ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miiko ya kazi katika utumishi wa umma ikiwamo utumiaji mbaya wa madaraka, mali za umma kama vile magari ya serikali na uzembe katika kutekeleza majukumu. Alisema hali hiyo inasababisha usumbufu kwa wananchi.

"Katika mkutano huu ningependa kusisitiza suala la nidhamu ya kazi na uwajibikaji. Uwazi na uwajibikaji ni msingi wa haki za binadamu na utawala wa sheria. Pamoja na hatua kubwa iliyofikiwa ya kujenga nidhamu katika utendaji kazi na uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma, bado wako watumishi wachache miongoni mwenu ambao hawawajibiki ipasavyo," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya uwajibikaji ili kuhakikisha kwamba viongozi na watumishi wa umma katika ngazi zote wanakuwa na malengo yanayopimika na yanayotekelezeka.

Aliwaagiza kusimamia mifumo ya kuboresha utendaji kazi serikalini ukiwamo mfumo wa wazi wa upimaji wa utendaji kazi na mkataba wa huduma kwa mteja ili kuhakikisha watumishi wote wanawajibika na kulipwa mishahara kwa kazi zenye matokeo na tija kwa wananchi.

"Pia ninawasisitiza kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na rushwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na katika utumishi wa umma kwa kukuza uwazi na uwajibikaji na ufanisi katika kutoa huduma," alisema.

Katika hatua nyingine, Mhagama aliagiza wahakikishe michango ya watumishi inawasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati na nyaraka zote zinazohitajika zinaandaliwa miezi sita kabla ya mtumishi kustaafu na stahili za wastaafu zinazotakiwa kutolewa na zitengewe fedha katika bajeti za ofisi zao kila mwaka.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri akizungumza na baadhi ya vijana kwenye eneo linalojengwa uwanja wa ndege wa kisasa lililopo Msalato Jijini Dodoma ambao walikuwa wakisubiri kupatiwa vibarua vya kujenga jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Silinde ataka barabara kufungwa taa

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, ameagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuzingatia maagizo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ya kila mradi wa barabara kuwa na kipengele cha ufungaji taa.

Silinde alitoa maagizo hayo jana wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa barabara ya urefu wa kilomita moja iliyojengwa na TARURA kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 400 kutoka serikalini.

Alisema tayari Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa alishatoa maagizo kwa miradi yote ya barabara kuzingatia kipengele cha ufungaji wa taa ili kubadilisha mandhari ya maeneo husika.

Akizungumzia ujenzi wa barabara hiyo, Silinde alisema ni lazima kabla ya kuzinduliwa iwe imefungwa taa.

"Ni lazima barabara hii ifungwe taa kama ambavyo Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa alishayatoa nikuagize Meneja wa TARURA wa Chamwino uhakikishe fedha kwa ajili ya ufungaji wa taa katika barabara hii zinapatikana ili hata tukimleta hapa kuja kuzindua, akute kumebadilika na panavutia," alisema Silinde.

Pia alisema serikali ina mpango wa kuongeza kilomita zingine kwa kiwango cha lami ili kulifanya eneo hilo kupanda hadhi kuwa mji mdogo.

"Katika mwaka huu wa fedha pia hapa mna kilomita moja ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini tutajitahidi pia kuongeza kilomita zingine tatu ili mpaka anamaliza muda wake mbunge wenu, tutakuwa tumeweka lami katika maeneo yote.

"Nitamwagiza Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Seif, kulifanyia kazi jambo hili na mimi ndiye nitakayelisimamia," alisisitiza Silinde

Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

"Mheshimiwa waziri tunakuomba utufikishie shukrani zetu kwa Rais kwa fedha alizotupatia kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo inakwenda kubadili mandhari ya eneo hili ambalo hivi sasa linakuwa kwa kasi," alisema.

Pia alisema eneo hilo hivi sasa linakuwa kwa kasi hivyo wanaiomba serikali kuendelea kuzifungua barabara ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa za kilimo ikiwamo zabibu pamoja na alizeti.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Chamwino, Mukandi Manga, alisema barabara hiyo iko katika hatua za mwisho kukamilika na agizo la ufungaji wa taa watalizingatia.





Omar Hamad mkulima wa mwani wa kijiji cha Tumbe, Pemba akipanda mwani katika shamba lake la mwani katika bahari ya Tumbe Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yatangaza mkakati kupambana na vitendo vya udhalilishaji, ubakaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetangaza mikakati ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuvitaka vyombo vya sheria kuharakisha uchunguzi wa kesi hizo na wahusika kufikishwa mahakamani haraka.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema Wizara hiyo ni mpya na imeundwa kwa ajili ya kushughulikia changamoto zinazowakabili wanawake, watoto, wazee na kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pembe alisema matukio ya udhalilishaji wa kijinsia kwa sasa yamechukua nafasi kubwa na Wizara imekuja na mikakati ya kuhakikisha yanashughulikiwa kwa sababu yanadhoofisha mustakabali wa maisha ya kundi hilo.

Alisema kwa mwaka 2021/22 matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji, yaliongezeka na kesi 373 zilipokewa katika vituo vya polisi na kufikishwa mahakamani.

Kwa upande wa Pemba, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia yameongezeka na kufikia 222 tofauti na Unguja ambapo kesi 151 zilipokewa.

Alisema kasi ya mwenendo wa usikilizaji wa kesi hizo imekuwa ikizorota kwa sababu mbalimbali ikiwamo familia kukubaliana na kuyamaliza matukio hayo kwa njia ya maelewano.

Pia alisema baadhi ya kesi zinamalizika kienyeji kwa wahusika wawili kufunga ndoa na hivyo inakuwa vigumu kuendelea na kesi hiyo mahakamani.

"Jumla ya kesi za udhalilishaji 100, wahusika walikubaliana kienyeji na kumalizana ikiwamo wengine kuoana, hatua ambayo inarudisha nyuma juhudi za kukabiliana na kesi za udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Waziri Pembe alisema serikali imefanya vikao na taasisi zinazoshughulikia sheria na mwenendo wa makosa ya jinai ikiwamo Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mahakama katika kuzishughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kusikilizwa kwa haraka.

Aliyataja baadhi ya makubaliano hayo kuwa ni kuhakikisha kesi zinachukuwa takriban muda wa miezi mitatu katika kukamilisha upelelezi na baadaye kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kutajwa.

Pembe alisema wizara imefanikiwa kuimarisha huduma za ushauri nasaha kwa kufuatilia wahanga wa matukio hayo ya kifamilia ikiwemo ndoa na talaka.

# Wataka mapitio sheria udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameitaka serikali kuangalia upya marekebisho ya Sheria ya Udhalilishaji wa Kijinsia kuona inawatia hatiani watuhumiwa wote wawili wa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia wakiwamo wanawake.

Waliyasema hayo katika kikao cha baraza la wawakilishi wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2022/23.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake Mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Khamis Hamad, alisema umefika kwa Sheria ya Udhalilishaji wa Kijinsia ambayo ilipitishwa na kuanza kutumika takriban miaka miwili, kufanyiwa marekebisho baada ya kujitokeza kasoro mbalimbali.

"Hivi sasa wanawake wamekuwa wakiwasingizia wanaume wanataka kuwabaka lakini ukiangalia ukweli unaona kwamba watu hao wamekubaliana lakini matokeo yake unakuta mtoto wa kiume ndiye anayekamatwa na kuwekwa rumande bila dhamana," alisema.

Naye Mwakilishi wa Gando, Mariyam Thani, alivitaka vyombo vya dola likiwamo Jeshi la Polisi kuacha kusuluhisha kesi za udhalilishaji wa kijinsia kienyeji na wakati mwengine kutoa kiwango cha fidia.

"Hili suala lipo linafahamika. Polisi wanasuluhisha kesi za udhalilishaji na wakati mwingine wanakwambia ni vyema mkamalizana kwa sababu kesi hii haiwezi kwenda popote," alisema.

Mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf, aliitaka wizara kuangalia suala la utelekezaji wa watoto na wanawake wakati ndoa inapovunjika ambapo wanawake wanapata mateso makubwa ikiwemo kupoteza kila kitu.

"Bado changamoto kubwa inayowakabili wanawake na watoto ni suala la utelekezwaji na talaka. Wizara inatakiwa kuweka mikakati madhubuti kupambana na wimbi la talaka kuona jamii ya wanawake na watoto wanaishi vizuri," alisema.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Annatas Paul, alisema wizara imeanzisha nyumba salama kwa ajili ya kuwapatia hifadhi wanawake na watoto waliopata matatizo ya udhalilishaji wa kijinsia ambapo nyumba hiyo ni siri na haitangazwi.

Alisema nyumba hiyo muundo wake ni wa siri na haitakiwi kufahamika na watu wa kawaida kwa sababu iko kwa ajili ya kuwapatia hifadhi na matunzo ya watu wanaopata matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

# Mabwawa 100 ufugaji wa majongoo bahari kujengwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu , inakusudia kujenga mabwawa 100 ya Majongoo bahari na mengine 40 ya kufuga samaki ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuongeza kiwango cha uzalishaji wa samaki kuelekea uvuvi wa mazao ya baharini.

Waziri wa wizara hiyo, Suleiman Masoud Makame, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu kazi zinazofanywa katika kuimarisha kilimo cha mazao ya baharini ikiwamo ufugaji wa majongoo bahari na samaki.

Alisema ufugaji wa mazao ya baharini yakiwamo majongoo bahari umepewa kipaumbele na kupitia fedha za UVIKO -19 zilitengwa Sh. bilioni 36. Kupitia fedha hizo, alisema wizara inakusudia kujenga mabwawa 100 kwa ufugaji wa majongoo bahari.

Waziri alisema kilimo cha ufugaji wa majongoo baharini hivi sasa kimekuwa na tija kubwa kutokana na umuhimu wake katika soko la kimataifa.

"Mheshimiwa Naibu Spika tunatarajia kujenga mabwawa 100 kwa ajili ya wafugaji wa mazao ya baharini aina ya majongoo, kilimo ambacho utafiti wetu tuliofanya kina tija kubwa," alisema.

Kuhusu ufugaji wa samaki, alisema wizara imejipanga kuhakikisha mabwawa 40 yanajengwa kwa ajili ya wafugaji samaki na kuona wanapata kipato kikubwa.

Alisema wafugaji samaki 1,427 wamejitokeza na mchakato wa awali ni kuwapatia mafunzo na mbinu za kisasa za ufugaji wa samaki wenye tija.



**ABAAH**

UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MEI 28, 2022



# WATAWEZA KUMFIKIA? Jibu lipo kwa Jux, Huddah

MWANAMUZIKI mkali wa miondoko ya kimapenzi, R&B, Juma Jux , maarufu kama The African Boy, ameibua maswali mengi kutoka kwa mashabiki wake baada ya kuwepo kwa tetesi kwamba anatoka kimapenzi na mrembo kutoka Kenya Huddah.

Huddah anayejulikana kama The Bosschick na Jux wameonekana kuwa karibu na kufanya mambo yenye hisia kali, kiasi ambacho kinawafanya watu kuwafuatilia kwa karibu.

Hata hivyo, baadhi ya mashabiki wameibuka katika mitandao ya kijamii wakisema kapo hiyo haitapendeza kama alivyokuwa na Vanessa Mdee.

Jux amemtumia Huddah kama 'Video Queen' wa ngoma yake ya 'Simuachi' ambapo wawili hao wameonekana kupendeza, lakini wengi wanadai kuna utofauti kati yao.

Hii sio mara ya kwanza kwa Jux kuhusishwa kuwa kwenye mahusiano na Huddah, story hizo zilianza baada ya Jux kuachana na Vanessa Mdee.



## BASI SAWA

## Ochieng awaimbia wanawake 'Hera Mbise'



MWIMBAJI wa muziki wenye asili kutoka Kenya, Alvaro Ochieng, ameachia wimbo wake mpya 'Hera Mbese' ambao ni maalumu kwa wanawake wanaolea vizuri watoto wao.

Alvaro amesema kuwa yupo kwenye harakati za kufuata nyayo za magwiji wa muziki huo kama Ochieng Kabaseleh, Johny Junior na Musa Juma.

Msanii huyo pia anatamba na nyimbo zingine Tina Molli, Aggrey Papa na Velonah Achieng.

"Hera Mbese ni wimbo ambao unawasifu akina mama kwa vitendo vya kijushaa kwenye jamii, unajua wakati mwingine wanaweka maisha yao kwenye hatari ili kuhakikisha watoto wanapata maisha mazuri." amesema

## Jerry A Brand awaambia 'Nimepona'



KINDA wa Bongo Fleva, Jerry A Brand, ameweka wazi kwamba ukimya wa muda mrefu umekwisha, sasa amerudi jukwaani kuwatuliza mashabiki kwa ngoma yake mpya inayoitwa 'Nimepona".

Akizungumza na BT, Jerry A, amesema alikuwaanajipanga katika projekti yake hiyo, hivyo mashabiki watarajie kuona uwekezaji mkubwa kwenye audio na video.

" Hii ni video ambayo nimetumia pesa nyingi na kufanywa na muongozaji mkubwa Ngota kwa ubora unaokubalika. Naamini mashabiki watafurahia na kuendelea kuniunga mkono muziki wangu ufike mbali, video inatoka Jumatatu kwenye chaneli yangu ya YouTube na TV mbalimbali," amesema Jerry A Brand.



## Kiba amlambisha ladha mwalimu wa mazoezi

UKITAKA kizuri lazima ukigharamikie! Ndivyo inavyoonekana kwa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Ali Kiba, baada ya mwalimu wake wa mazoezi Denzel Trainer, kuanza kula matunda.

Hivi karibuni, Denzel amesema alisafiri hadi Afrika Kusini kwa ajili ya kuongeza ujuzi ili kumfanya mwanamuziki huyo awe na muonekano mzuri na usiochuja.

"Mimi na Alikiba tumeanza kufanya kazi mwaka jana, lakini nafurahia kuwa naye kutokana na juhudi zake za kunifanya niwe mkufunzi mkubwa na mwenye sifa zote," amesema.

# Busumba: Ahadi ya uongo, nyota shahidi

**Na Adam Fungamwango**

BUSUMBA ni filamu ya kusikitisha sana ya mapenzi inayomhusu kijana John aliyempenda sana mkewe Matha.

Udhaifu wa mwanaume kwenye penzi la mkewe, ndiyo unaomuangamiza.

Imechezwa na Kulwa Mguti, Doto Mguti, Nasri Khamisi, Alex Alex na Martha Bernard.

John na mkewe wapo barazani wakipeana ahadi mbalimbali za kimapenzi. Ndoa changa na penzi shatashata.

Mkongano na msuguano kwenye mapenzi au ndoa upo, lakini watu hukaa na kuyasuluhisha.

Hata hivyo kuna watu wabaya walichukua udhaifu huo wa msuguano wao kuiua ndoa hiyo na kusababisha maafa.

Licha za ahadi za 'nakupenda kuliko kitu chochote duniani' Matha, mke wa John anakutana na kijana mwenye 'lugha ya miujiza' na kushawishi kimapenzi.

Nyumba sasa ikawa haikaliki. Hakupikiki wala hakulaliki, kila siku kiguu na njia kwenda kwa kijana 'Lover Boy'.

Kwanza alitoroka na kwenda huko, lakini akarudi na kumuomba msamaha mumewe. Akasamehewa, akatoroka kwa mara ya pili.

John anapigiwa simu na mtu asiyejulikana na kumwambia kuwa mkewe anaye yeye. Kwa kujua kuwa anampenda mkewe akalazimisha afanye mambo kadhaa ya hatari, ili ampate mkewe.

Kwanza akamlazimisha akampore mtu begi la pesa na kwenda kuliweka sehemu fulani. Halafu akamlazimisha akaue. Na kila akitaka kukataa, anaambiwa kuwa mkewe atauawa. Anatekeleza kila kitu alichoambiwa.

Mwisho anaambiwa kule ambako atamkuta mkewe. Ni kweli akamkuta, lakini kitu anachokikuta haamini macho yake.

Kumbe yule aliyekuwa akimtuma ndiye mpenzi wa mkewe. Na ilionekana hivyo hata mbele yake. Na hata mkewe alionyesha kuwa na mapenzi na jamaa huyo, kwani walianza kuonyeshana mbele yake. Na ilionekana hivyo hata mbele yake. Kwa hasira kwa sababu alikuwa na kisu akajaribu kupambana na jamaa, lakini kisu kilifika na kuua mkewe.

Baada ya hapo hakuwa kwenye wakati mzuri, mawazo ya kumkumbuka mkewe, pamoja na kufikiria ni kwa nini alimsaliti.

Ikamsabishia ugonjwa wa akili na kuanza kuishi kwenye majumba mabovu na jalalani. Hiyo ikawa ndiyo maisha yake.

Kuna siku alikutana na jamaa wakiwa wanataka kupigana kwa kudhulumiana. Akawasihi wasifanye hivyo kwa maneno matamu. Akawa rafiki yao na kumkaribisha kwenye gheto lao.

John akili haikukaa sawa, akaanza kuumwa. Wakati rafiki zake wakitaka kumpeleka hospitali, aliwaambia kuwa hatopona, na akifa, azikwe jalalani. Akafariki dunia siku chache baadaye na akazikwa kama alivyoagiza mwenyewe.





## Kumbe 'Naogopa' ingekuwa vingine

Je umeisikia ngoma ya 'Naogopa' ambayo amefanya Marioo na Harmonize? Kama umeilewa vizuri basi, mapigo yale yalikuwa ya Jux kama mambo yasingeharibika.

Mtayarishaji maarufu wa muziki,Abbah Process, amesema ngoma hiyo ilitengenezwa kwa ajili ya mwanamuziki huyo wa muziki wa mahaba, lakini hakuwa vizuri kutokana na uchovu, hivyo alishindwa kuweka sauti.

"Hii biti ya Naogopa mara ya kwanza nilifanya na Jux, baada ya kuitengeneza alikuwa hana 'Mudi' kwa sababu alikuwa amechoka, kila tukipanga tufanye kinatokea hichi mara kile," amesema

## PENZI LIKIISHA NI SUMU

**Na Adam Fungamwango**

PENZI ni kitu cha ajabu sana duniani. Kinampa binadamu furaha, amani, utulivu na kila aina ya faraja.

Anayependa au kupendwa anatamani aote mbawa kama ndege apae angani na kuitangazia dunia nzima jinsi gani anapendwa au kupenda.

Ndiyo wakati ambao hakuna yoyote anayeona mapungufu au kasoro yoyote ya mwili na tabia.

Kwenye pengo huona kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.

Mwenye kupenda haoni wala hasikii. Penzi ni dawa.

Kwa bahati mbaya ikitokea likiisha ndipo hapo linapokuwa sumu. Kuna watu dunia wanaiona chungu. Wanaona hata dunia yenyewe si sehemu salama ya kuishi. Baadhi wanaishia kujinyonga. Na hata ambao hawafanyi hivyo wanachukua muda mrefu hadi kurejea kwenye hali ya kawaida, inategemea na kichwa cha mtu mwenyewe. Hiyo ni baada ya 'kupigwa chini' au kuamua kuacha mwenyewe kwa sababu mbalimbali, kuu ni kutendwa.

Hapa leo tunaangalia nyimbo za dansi ambazo zinaonyesha penzi linapokuwa limefikia ukingoni, liwe la mke na mume, au wapenzi.

**Solemba-Juwata Jazz Band**

Huu ni wimbo wa Juwata Jazz Band uliorekodiwa mwaka 1985, ukitungwa na kuimbwa na mwanamuziki mlemavu wa macho, Nico Zengekala aliyefariki miaka miwili baada ya kutoa wimbo huo 'Solemba'.

Unamzungumzia mtu mmoja ambaye ameamua mwenyewe kulivua penzi, baada ya mwanamama aliyempenda kuonyesha kuwa hana habari naye.

Jamaa alienda nyumbani kwa 'demu', lakini badala ya kukaribishwa 'akachomeshwa mahindi', kuanzia asubuhi hadi saa nane jua likimuunguza.

Akarudi nyumbani kwa kuamua kuwa liwalo na liwe lile penzi basi.

**Tereza-Vijana Jazz Band**

Huyu jamaa ndiyo anatia huruma kabisa. Huyu akakataliwa siku ya harusi mbele ya kasisi na jamaa na marafiki waliofika kwenye sherehe hizo. Hebu pata picha aibu yake ikoje?

Mwanamama anaitwa 'Tereza'. Alikuwa mpenzi wake na akakubali kabisa kuolewa. Alichokifanya siku ya harusi kimebaki kuwa historia.

Wimbo ulitungwa na kuimbwa na Jerry Nashon mwaka 1990, akiwa na Vijana Jazz Band.

**Edita-DDC Mlimani Park**

Kuna vitu vingine vya kusikitisha sana. Kwenye wimbo huu, jamaa anamlalamikia mpenzi wake anayeishi naye nyumba moja, kumsaliti na kumletea mwanaume ndani ya nyumba yake.

Jamaa kila siku anaambiwa kuwa mpenzi wako si mwaminifu, lakini alijua ni fitina tu za majirani. Kila anaporudi kazini hamkuti, akimuuliza anaambiwa alikwenda kwa shangazi yake kariakoo, kumbe yupo na bwana. Siku alipomfuma ndani ndiyo yalipomshinda, akanawa maji.

Umetungwa na kuimbwa na Hassan Rehani Bitchuka akiwa na DDC Mlimani Park, katikati ya miaka ya 1980.

**Makumbele-Maquiz Original**

'Makumbele' ni wimbo wa miaka ya mwanzoni mwa 1990, utunzi wake mpiga 'trumpet' Kaumba Kalemba.

Unamzungumzia, mama mmoja anayemlalamikia mume wake ambaye amemfanyia mambo mengi mabaya, lakini sasa imetosha, amefika mwisho anarudi kwa baba na mama yake.

**Siwema-Dar International**

Wimbo huu wa miaka ya 1980, ulitungwa na Marijani Rajab akiwa na bendi ya Dar International. Unazungumzia jamaa mmoja akimlalamikia mpenzi wake Siwema ambaye kumpenda kwake kukafanya kumtangazia kuwa amemuweka kwenye kiganja.

Jamaa kashtuka, kaanza kumwambia kuwa yeye hababaiki na sura, anapenda tabia njema tu.



## Cannon watoto ni zawadi

MWIGIZAJI wa Marekani na mtangazaji wa TV, Nick Cannon, amefichua kuwa anafikiria kufanya upasuaji kufunga uzazi 'vasektomi' ili apate muda wa kuwalea watoto wake saba.

"Tayari nilikwenda na kupata ushauri wa vasektomi. Sitazamii kujaza Dunia kabisa, lakini kwa hakika ninatazamia kuwatunza na kuwapenda watoto wote ambao ninao kwa sasa," amesema.

Cannon amekuwa na tahadhari kubwa kutokana na uwezo wake mkubwa kupata watoto kwa kila mwanamke aliyejihusisha naye kimapenzi na sasa ameamua kufunga uzazi kabisa.




## Miss England alalama kubaguliwa

MSHINDI wa taji la Miss England 2021, Rehema Muthamia, amesema amewahi kubaguliwa kutokana na rangi yake nyeusi, wiki kadhaa kabla ya kushinda taji hilo.

Rehema (26) ambaye ana asili ya Kenya,ameliambia gazeti la Daily Mail kuwa amewahi kuulizwa maswali mengi kwa nini Mwafrika anaweza kuwa Miss England.


"Tarari nilijua nitaangaziwa katika ubaguzi kama mwanamke mweusi ndani ya Uingereza, sio London kunamengi hapa nchini kama mwanamke mwenye asili ya Kiafrika anakabiliana na watu wananifuata," amesema.

## Kumbe Kourtney mke halali wa Travis

NYOTA wa kipindi cha maisha halisi cha televisheni Marekani, Kourtney Kardashian, imeelezwa amefunga ndoa na mpenzi wake Travis Baker.

Mrembo huyo maarufu na mchumba wake walifunga pingu za maisha huko Santa Barbara, California siku ya Jumapili iliyopita.

Kulingana na PageSix, Wawili hao walionekana wakiwa wamevalia mavazi ya kitamaduni ya harusi katika mahakama ya jiji la Anacapa.





## Trevor, Minka kisicho ridhiki hakiliki

MCHEKESHAJI wa Afrika Kusini Trevor Noah na mpenzi wake, Minka Kelly, hatimaye wameachana baada ya kuwa pamoja kwa muda wa miaka miwili.

"Minka yuko singo," kilisema chanzo kimoja na kuongeza kwamba mrembo huyo ana furaha zaidi baada ya kuachana na msanii huyo wa uchekeshaji.

Chanzo kingine kilisema Kelly na Noah wamethibitisha kwamba penzi lao limesambaratika muda mrefu.

## Leo Mesie afariki dunia

MSANII wa filamu wa Nigeria, Leo Mezie amefariki dunia baada ya kusumbuliwa na tatizo la figo kwa muda mrefu.

Kifo hicho kimethibitishwa na rafiki yake mkubwa, Chioma Topis kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Mwigizaji Leo Mezie amefariki Jumapili huko Abuja wakati akipatiwa matibabu ya kibofu. Alifikishwa hapo akitokea nyumbani kwake Umuahia. RIP Leo," ameandika Chioma.

Kabla ya kifo chake, Leo alikwenda Uingereza kupata matibabu mwaka 2016, na aliporudi Nigeria hali yake iliimarika na kuendelea na shughuli zake.



**MAKALA**

# Dk. Gwajima anapokerwa wazazi wanaonyanyasa watoto nyumbani

## ●Wadau watoa ya moyoni walia na malezi duni

**Sabato Kasika**

WATOTO wanakabiliwa na hali ya ukandamizwaji na unyanyaswaji unaofanywa na wazazi, walezi na marafiki ndani ya familia.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akifungua mkutano wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) Mkoa wa Dar e s Salaam hivi karibuni.

Waziri aliwataka wajumbe kuandaa mkakati madhubuti utakaosaidia kuimarisha ulinzi wa watoto kwa lengo la kutokomeza vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

Mkutano huo uliwashirikisha wadau mbalimbali, wakiwamo viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya chini, askari polisi, wanafunzi, maofisa afya, maofisa wa maendeleo ya jamii, wazazi na wengine wengi.

Dk. Gwajima anasema, Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto ndani ya mkoa zinatakiwa kukamilisha uundwaji wake katika kujijengea uwezo ili ziweze kutekeleza majukumu ipasavyo.

"Katika mkutano huu, hakikisheni mnakuja na jibu ambalo litasaidia kufanikiwa katika vita hii ya kupambana na ukatili, kwani vita yenyewe inahitaji kujitoa zaidi, " anasema Waziri Dk. Gwajima.

Anafafanua kuwa katika mazingira hayo, baadhi yao wamekuwa wakikimbia kweye nyumba zao na kudandia magari kwenda mijini na kujikuta wakilala katika vituo vya mabasi na wengine chini ya madaraja, jambo ambalo si zuri katika ustawi wa watoto.

"Wapo baadhi ya wazazi hawawalei vizuri watoto wao hali ambayo inawafanya wajihusishe na vitendo vya uhalifu vikiwamo kujiunda kwenye makundi kama 'panya road'. Wale wasiosimamia malezi bora tutashughulika nao," anasema.

Waziri huyo anaeleza kwamba bila kamati hiyo ngazi ya mkoa kubuni mikakati zaidi ya kutambua changamoto zinazowakabili watoto, nchi inaweza kujikuta ikiongozwa na watu wasio na maadili mema.

Anatoa wito kwa kamati za MTAKUWWA kote nchini kuhakikisha zinafuatilia na kutambua idadi ya watoto kuanzia ngazi ya vitongoji pamoja na changamoto zao na kuzifanyia kazi haraka kabla hawajachukua hatua ya kukimbilia mitaani.

Anasema ni muhimu wadau kutekeleza hatua zinazolenga kupambana na vitendo vya ukatili.

"Nitoe wito kwa wanaume, msitelekeze watoto wenu, mnachangia kuwapo kwa watoto wanaozurura mitaani, serikali inataka kuwa na taifa bora, hivyo hakikisheni mnasimamia malezi bora ya watoto wenu," anasema.

Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula anakemea watu kutumia jina la watoto wa mitaani, kwa madai kwamba hakuna mtoto wa mtaani, bali kila mmoja ana wazazi wake na kutaka jamii iwatambue na kuwasaidia.



Mkuu wa Polisi Wilaya ya Chang'ombe (OCD) SSP Ariziki Makwaya, akizungumza kwenye mkutano huo. Kushoto ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima na Mkuu wa Wilaya ya Temeke Jokate Mwegelo. **PICHA: SABATO KASIKA**

**HALI ILIVYO DAR**

Katika Mkoa wa Dar es Salaam idadi ya watu ni zaidi ya milioni 6, unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kuwa na watoto wengi wanaoishi na kufanya kazi mbalimbali kinyume na sheria ya mtoto.

Kulingana na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulid, watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni 2,984.

Aidha, katika idadi hiyo, watoto wa kiume ni 2,114 na wa kike 780 ikiwa ni sawa na asilimia 50 ya watoto wote wanaoishi na kufanya kazi mitaani nchini kote.

"Watoto hao wanafanyishwa kazi mbalimbali ikiwamo biashara ya kuokota chupa za maji, vyuma chakavu, kuosha magari, lakini mbaya zaidi kufanyishwa biashara ya ngono na wale wanaowamiliki," anasema Maulid.

Anaongeza kuwa wengine wamegeuka kuwa ombaomba huku wakiwa na wazazi ama walezi wao, na kwamba yote hayo yanatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo umaskini wa familia na migogoro ya ndoa.

"Sababu nyingine ni kukosa usimamizi, ukatili uliokithiri, vifo vya wazazi, kuwa na matamanio ya maisha wanapoona wenzao wana vitu wanatamani na kujiingiza kwenye shughuli mbalimbali ili kupata fedha," anaongeza

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Lilian Chilo anasema jamii imesahau jukumu la malezi, badala yake watoto wanafanya matendo mabaya hakuna wa kukemea.

"Wazazi na walezi nao siku hizi wamekuwa ni watu wa kutunza siyo kulea ili watoto wawe na maadili mema, na ikumbukwe kuwa watoto wana malengo yao lakini hawawezi kuyafikia kama hawana malezi bora," anasema Chillo.

Aidha, anasema ipo haja ya kuwa na kituo maalum cha kupokea watoto wa mitaani wakati mikakati ya kujenga vituo zaidi ikiendelea ili kuwaondoa mitaani ambako wamekuwa wakizurura kutafuta fedha.

"Lakini jambo hili lifanyike kwa umakini ikiwamo kuwachunguza ili wasiende katika kituo na kufanya ukatili kwa wenzao au kuiba vitu. Ninaamini vituo vingi haviwapokei kwa kuhofia mambo kama hayo," anasisitiza.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Chang'ombe (OCD) SSP Ariziki Makwaya, anasema bado kuna haja ya kuwa na nyumba salama nyingi ili kusaidia manusura wa vitendo vya ukatili.

Anasema, waathirika wanapofika au kufikishwa kituo cha polisi wanatakiwa wasirudi maeneo ambayo yamemsababishia hatari, na kwamba baadhi yao wanalazimika kurudi kutokana na ukosefu wa nyumba salama.

"Kuwapo kwa nyumba salama nyingi kunaweza kuwasaidia manusura, hivyo mheshimiwa waziri huo ndio ushauri wangu kwamba kuwapo na mkakati wa kuhakikisha nyumba hizo zinajengwa," OCD Arikizi anasema.



Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Lilian Chilo akichangia mada kwenye mkutano huo: **PICHA: SABATO KASIKA**

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Watoto walivyoogeshwa zamani

## •Ndoo ya bati, sabuni mchubuo
## •Fumba macho, inua mguu, legeza mwili

**Na Adam Fungamwango**

KUNA shabiki mmoja wa makala hii alinipigia simu kutoka mkoani Kilimanjaro, ambapo mbali na mambo mengine mengi yaliyomkosha kuhusu vitu mbalimbali ambavyo vimekuwa vikimkumbusha enzi ambazo alikuwa mdogo, alikumbushia jinsi watoto walivyokuwa wakiogeshwa zamani.

Alinikumbusha vitu mbalimbali hatua moja baada ya nyingine ambapo kinamama wa zamani walikuwa wakiwaogesha watoto wao. Alichoeleza ni kweli kabisa. Siku hizi watoto kuanzia miaka minne hadi saba wamekuwa wakiogeshwa kwa kubembelezwa.

Na inawezekana asilimia kubwa hawaogeshwi na wazazi wao kama zamani, bali madada wa kazi.

Nadhani kwa sababu madada wao wako kazini, wamekuwa wakiwaogesha kwa namna ya kubembelezwa zaidi.

Na hata wazazi wa sasa ambao wamekuwa wakiwaogesha watoto zao, hawatofautiani na madada wa kazi.

Ni tofauti na zamani. Watoto walikuwa wanaogeshwa kama wako jeshini. Cha ajabu ilikuwa ni kama mfumo hivi.

Anayeogeshwa na mama yake anaweza kuona kama mama yake 'mnoko', lakini akienda kwa rafiki yake atamkuta naye anaogeshwa kwa namna ile ile, au zaidi. Ni kama walikuwa wameambizana hivi. Kinamama wengi walikuwa na tabia hiyo hiyo wanapoogesha watoto.

Ikafikia wakati watoto wote wakadhani ili uogeshwe ni lazima ufanyiwe hivyo. Miaka ya zamani kuanzia 1990 na kurudi nyuma, mara nyingi watoto walikuwa watundu mno kiasi kwamba walioga mara moja au mbili tu, asubuhi wakati wa kwenda shule, na saa 11:00 jioni au saa 12:00 jioni.

Picha linaanza kwanza ikifika jioni akinamama wanaanza kuwatafuta watoto wao. "Umeniona Kassim hapa?" Mmoja wa akinamama atakuwa anauliza majirani.

Kama nilivyosema watoto wa miaka hiyo walikuwa watundu na watembezi, na si rahisi kumuona amekaa sehemu moja kwa muda mrefu, haswa wa kiume.

Anapopatikana kwanza anaanza kwa kuchapwa kibao, kabla ya kutiwa mkononi na kurudishwa nyumbani, tayari kwa kuoga.

Ukimuona mtoto na mama yake, ni kama mchungaji anampeleka mbuzi machinjioni, jinsi alivyomshika na kurudi naye nyumbani.

Kwanza mtoto keshakula kibao, halafu haikuwa rahisi sana watoto zamani kukubali kuoga bila kushurutishwa, kupigwa, au kubembelezwa. Kuoga ilikuwa ni tatizo kubwa.



Ukifika kwanza unapelekwa kwenye beseni au ndoo ya bati, iliyokuwa imejazwa maji nusu.

Unaambiwa uingie, na kazi ya kuogeshwa ndipo inapoanza. Baada ya kuinadi mada hiyo kwa wadau, ni kama vile niliweka ndimu kwenye mboga, maana ilimwinua kila mmoja kwa staili yake, akiwa na mchapo wa kukuacha hoi kwa yale ya zama zake.

Sasa naamini ya kale dhahabu. Nilianza kwanza na shabiki huyo wa Kilimanjaro, yeye akanimegea hivi kuhusu namna ya kuogeshwa: "Nishike kichwani! Unasuguliwa miguu mpaka unasema hiki nini, unaoshwa kama gari..."

Mwenzake naye akadakia na kipengele chake "Chuchumaa chini haya, penga kamasi tena penga fumba macho..., simama pale ukauke kwanza, jamani!" Huku wenzake wakiendeleza yake yaliyomkuta, hivi.

**Na hata wazazi wa sasa ambao wamekuwa wakiwaogesha watoto zao, hawatofautiani na madada wa kazi.**



"Fumba macho, inua mguu, panua mabega, ukiteleza unasindikizwa na kibao au kofi la mgongo, ukiyumba unapata la kibao kichwani, ukitoka hapo mwili unawaka moto unabaki unasinzia kusubiri chakula cha usiku, du!"

Naam hayo ndiyo mambo ya enzi hizo. Hayajaisha, hebu pata ya huyu: "Unaambiwa funga mdomo usinywe maji! Maana unakuta umeshayakojolea, kwenye ndoo ya bati na sabuni ya kipande ya njano."

"Kuoga nilikuona kuchungu mwee! Halafu kuna kijiwe fulani hivi, ambako Bi. mkubwa alikuwa anasugulia miguu akitoka bafuni...tumepitia magumu hasa ukiogeshwa usiku utajua hujui."

Msikilize huyu na yake ya aina yake."Halafu ukute maji yenyewe ya baridi, weee, siku akishinda vizuri, anakuogesha juani ili usipate baridi. Hadi kigunzi cha mahindi watu tumesuguliwa, ukitoka hapo unawaka kama sufuria imesuguliwa na mchanga."

Wapo wadau wengine wanasimulia, walikuwa na yao tofauti zaidi kwa staili hii."...halafu ukute mama 'mnoko', kama mama yangu anakuacha na mapovu usoni mpaka amalize kuusugua mwili mzima, yaani hapo tu ndiyo nilikuwa sitamani kuoga, daah!"

Staili ya kutakatisha iko hivi, mdau anafunguka. "Halafu ukiwa unasuguliwa na yale madodoki ya magunia mgongoni unasikia maumivu kweli, ukianza kuugulia maumivu au ka-mgongo kajikunje kidogo, unapewa bonge la bao au unaambiwa kimya nasema 'kimya mbwa weeh!', ukishamalizwa kusuguliwa unageuzwa geuzwa kama chapati, ukimwagiwa maji ukiteleza tu, kofi...'hivi hulagi mbwa we'..."

Lakini, sifa moja ya watoto wa zama hizo nao walikuwa 'ngangari', wakikabiliana na hali hiyo, utundu kwa kwenda mbele, walichukulia hali hiyo ni kama sehemu ya maisha, wakibuni mbinu ya kupambana nayo, wakitoka michezoni, wanakwepa kuoga hadi 'wanaponaswa na trafiki' siku nne baadaye.

Hapo ndipo mdau anakumbuka shughuli pevu ya trafiki mama, akisimulia.

"Baada ya siku nne hivi ndiyo ukishikwa hali inakuwa hivyo, hapo ushakula fimbo zako unasuguliwa ukitoka hapo lazima ujue ngozi pia ni mlango wa fahamu, moto unaokuwakia!"

Mwingine naye alitoa yake kwa kusema "Umenikumbusha mbali, yaani ilikuwa ikifika muda wa kuoga ni tatizo sana, umesha ruka kwenye vumbi, mchanga kichwani kwenye nywele lakini ikifika kuoga ni kulia, eti mbona jana nilioga na leo nioge tena? Kila siku mimi tu, hahaha..."

Suala la kuachwa na sabuni kichwani lilionekana kuwakera watoto wengi sana wa zamani, leo wanafunguka kama huyu mmoja.

"Halafu ilikuwa kama makusudi fulani, unaachwa na hiyo sabuni hadi unakoma, jamani.

Nilikua naogeshwa kwa maji baridi na nikilia kuwa maji ni ya baridi mama alikua ananiuliza kwani vumbi nililochezea lilikua la moto?"

Kuna mmoja yeye akakumbusha akinamama 'wanoko', walivyokuwa wanawarudisha watoto ambao walipewa upendeleo na kuoga wenyewe.

"Kweli tumetoka mbali yaani sidhani kama kuna ambaye hajapitia, umenikumbusha mbali sana na siku ukipewa nafasi ya dhahabu ya kuoga mwenyewe penda usipende utarudishwa tu bafuni maana hutokuwa umeoga vizuri na lazima ukaguliwe na mama."

## Jeshi la DR Congo lawafukuza waasi wa M23

**GOMA,** DRC

RIPOTI za vyombo vya habari zinaeleza jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) limefanikiwa kuchukua na kudhibiti eneo la Jimbo la Kivu Kaskazini.

Eneo hilo lilitekwa na waasi wa M23, moja ya kundi lenye silaha za kisasa ambalo linaendesha operesheni zake katika eneo hilo la mashariki mwa nchi hiyo.

Radio Okapi inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa, iliripoti kwamba Vikosi vya Wanajeshi vya DR Congo vimechukua tena eneo la Kabaya, ambalo lina vijiji vya Kisigari, juzi.

Iliongeza kuwa jeshi limewarudisha nyuma waasi wa M23, ambao walikuwa wakitishia kuizingira kambi ya kijeshi ya Rumangabo, ambayo hapo awali iliripotiwa kutekwa na waasi hao.

Mapigano yalizuka mapema wiki hii katika maeneo kadhaa huko Kivu Kaskazini, ambayo inapakana na Rwanda.

Kufuatia uvamizi huo wa waasi, Marekani ilitoa ushauri ikiwaonya raia wake dhidi ya kusafiri katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo yenye utajiri wa madini.

Kundi la waasi la M23 - ambalo kimsingi ni la Watutsi wa Congo lilianza tena mapigano mwaka huu, likiituhumu serikali ya DR Congo kwa kushindwa kuheshimu makubaliano ya mwaka 2009 ambapo wapiganaji wake walipaswa kuunganishwa katika jeshi.

Wakati huo huo, DR Congo inaishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Christophe Lutundula Apala Pen'Apala jana aliishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi hao.

"Rwanda inasonga mbele naweza kusema bila kusita, Rwanda imeshambulia kambi ya Rumangabo huko DR Congo, narudia tena M23 wakiungwa mkono na Rwanda walishambulia wanajeshi wa kimataifa wa Monusco," Lutundula Pen'Apala alisema wakati wa mkutano wa Baraza Kuu la AU.

Uhusiano kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda ulikuwa umeanza kudorora baada ya Rais Felix Tshisekedi, kuchukua madaraka mwaka wa 2019, lakini kuzuka upya kwa ghasia za M23 kumeongeza hali ya wasiwasi.

**BBC**

# Vikosi vya Russia vyaingia viunga vya mji muhimu wa Severodonetsk

**KYIV,** UKRAINE

MAPIGANO makali yanaendelea katika viunga vya mji wa Severodonetsk, eneo muhimu linalolengwa na vikosi vya Russia vikijaribu kuuteka ili kudhibiti jimbo la Luhansk nchini Ukraine.

Mji huo umekumbwa na mashambulio ya makombora yanayoendelea na kusababisha asilimia 60 ya nyumba kuharibiwa kabisa.

Raia wanne wameuawa katika mapigano hayo, na kufikisha jumla ya watu wapatao 1,500 waliouwa tangu ulipoanza uvamizi wa kijeshi mwezi wa Februari mwaka huu.

**ZELENSKY: VITENDO VYA DONBAS NI MAUAJI YA HALAIKI**

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amedai mashambulio makali yanayofanywa na Russia katika eneo la Donbas mashariki mwa nchi hiyo yanaonyesha sera ya wazi ya mauaji ya halaiki.

"Mashambulizi ya sasa ya wavamizi huko Donbas yanaweza kufanya eneo hilo kutokuwa na watu, wanataka kuchoma Popasna, Bakhmut, Lyman, Lysychansk na Severodonetsk kuwa majivu," alisema Zelensky.

"Katika miji iliyo karibu na mpaka wa Russia kama Donetsk na Luhansk, vikosi vya Russia vinakusanya kila mtu wawezavyo ili kujaza mahali pa wale waliouawa na kujeruhiwa katika uvamizi," aliongeza Zelensky.

Alisisitiza kwamba matendo hayo ni pamoja na kufukuzwa kwa watu na mauaji ya halaiki ya raia, ni sera ya wazi ya mauaji ya halaiki inayofamywa na vikosi vya Russia.

Zelensky alitaka shinikizo kuwekwa kwa Russia kihalisi katika kuokoa maisha na kwamba kila kucheleweshwa pendekezo la kutuliza Russia Waukreni huuawa.

**VIFARU VYA ZAMANI VYAASHIRIA UKOSEFU WA VIFAA**

Jeshi la Russia linaaminika kutumia vifaru vya miaka 50 katika juhudi zake za kuteka eneo la kusini mwa Ukraine.

Magari aina ya T-62 yalipelekwa kuimarisha kikosi chake cha kusini, hayo kulingana na taarifa kutoka Wizara ya Ulinzi ya Uingereza (MoD).

Magari hayo yanafikiriwa kuwa yanaweza kuathiriwa na silaha za kukinga vifaru na inatokana na uhaba wa vifaa vya kisasa, vilivyo tayari kupigana.

Wizara ya ulinzi pia ilisema vikosi vya Russia vinaendelea na juhudi za kuzingira Severodonetsk na Lysychansk.

Hivi karibuni wameteka vijiji kadhaa kaskazini-mashariki mwa Popasna, lakini upinzani wa Ukraine unainyima Russia udhibiti kamili wa eneo la mashariki la Donbas.

Alisema vikosi vya Russia vilijaribu kuingia kwa nguvu wakati vikitokea miji iliyopo karibu ya Purdivka na Shchedryshcheve, na kushambulia ngome za wanajeshi wa Ukraine.

Vikosi hivyo vilikuwa vikifanya mashambulio ya hapa na pale dhidi ya maeneo yenye ulinzi mkali wa Waukraine katika Donbas tangu ilipoimarisha juhudi zake za kivita.

**BBC**




Wanajeshi wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo wakiwa katika harakati za kupigana na waasi wa kundi la M23 lilovamia Kivu Kaskazini hivi karibuni. **PICHA: BBC**

# Mwanamke mjamzito atolewa figo kwa siri

**KAMPALA,** UGANDA

POLISI katika wilaya ya Mubende nchini Uganda, wanachunguza tukio la madaktari kutoa figo ya mama mjamzito kwa siri.

Mjamzito huyo Peragiya Muragijemana ( 20) mkazi wa Kijiji cha Lwemiggo, wilayani Mubende, alielezea jinsi alivyokimbizwa hospitalini akiwa katika hali mbaya na kuhitajika kufanyiwa upasuaji, lakini figo yake ikadaiwa kuondolewa.

Muragijemana alisema alijifungua mikononi mwa mkunga wa jadi, lakini alishindwa kutoa kondo la nyuma, na kusababisha kutokwa na damu nyingi.

"Nilipelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa ya Mubende, ambapo mume wangu, Amos Tiringanya, alitakiwa kusaini hati ya kuniruhusu kufanyiwa upasuaji," alisema katika mahojiano na gazeti la Daily Monitor.

Mume wake alisema kuwa madaktari walimueleza kuwa ndiyo njia pekee ya kuokoa maisha yake kwani alikuwa akivuja damu.

"Baada ya upasuaji, mke wangu alirudishwa wodini akiwa amepoteza fahamu na aliruhusiwa baada ya siku tatu kutokana na msongamano hospitalini. Tulimpeleka nyumbani kwa mama mkwe wangu ," alisema.

Aliongeza: "Lakini baada ya siku tatu, nilipigiwa simu na mama mkwe akinijulisha kuwa mke wangu amepata matatizo ya tumbo. Tulienda kwa uchunguzi wa juu ambao ulionyesha kuwa figo yake ya kulia haikuwepo. Nilitia saini tu hati inayokubali kuondolewa kwa uterasi ya mke wangu ili kuokoa maisha yake, si figo yake."

Mama yake Musanabeera, alitoa taarifa polisi kufanya uchunguzi wa kina kuhusu madaktari waliodaiwa kutoa figo ya binti yake.

Dkt Onesmus Kibaya, msimamizi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mubende, alishauri familia ya Muragijemana kuwa watulivu kwani hospitali hiyo pia inafanya uchunguzi wake.

Anaeleza kuwa mwanamke anapokuwa mjamzito, viungo vikuu hupata matatizo. Viungo hivyo ni pamoja na moyo, figo na uterasi.

"Mbali na hilo, hospitali ya Mubende haina uwezo wa kufanya upasuaji wa figo bali hufanywa katika hospitali ya Mulago".

Msemaji wa polisi wa mkoa wa Wamala, Rachel Kawala, alisema wamechukua taarifa za mgonjwa na uchunguzi wa kisa hicho unaendelea. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**THE COMPANIES ACT**
**(CAP.212 R.E 2002)**
**ROAD TRIP TANZANIA LIMITED**
**BOARD RESOLUTION**

At a duly convened and constitute Board of Directors meeting of **ROAD TRIP TANZANIA LIMITED** through Skype on the 10, April,2019 at 10:00 am.

**PRESENT**

| | | |
|---|---|---|
| 1.JEAN DU PLESSIS | - | DIRECTOR |
| 2.OKKE DE BACKER | - | DIRECTOR |
| 3.LAURA VAN DIJK | - | DIRECTOR |
| 4.ANDREW BANNAN | - | SECRETARY |

**AGENDA**

**1. WINDING UP THE COMPANY**

Members have unanimously resolved that, they should **voluntarily wind up** the company because the company has ceased all its operations.

**2. APPOINTMENT OF AN ADVOCATE**

Members unanimously agreed that, they should appoint Advocate Marcelina John Bandiye from H&M Attorneys at Law, a law firm based in Arusha to oversee the whole process of winding up the company.

CERTIFIED TRUE EXTRACT
(By Order of the Board)

Dated at Arusha this 10th April, 2019.

JEAN DU PLESSIS — OKKE DE BACKER

LAURA VAN DIJK — ANDREW BANNAN

---

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/256/A/TUNGI**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: ALLY ATHUMAN MPANGILE WA S.L.P 5335 ,MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.256 KITALU "A" ENEO LA TUNGI MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: ALLY ATHUMAN MPANGILE S.L.P 5335,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa Mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA –MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO

VALENCY HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 54 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late PAULO ELIAS MAGESA MAKORO**

**By 1. DENIS ELIAS MAGESA**
**2.**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 31st day of MAY ..... 2022

Dated at MOROGORO this 12 day of MAY ...2022

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
Morogoro

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**RULES 13 CIVIL PROCEDURE SUMMONS AND PLEADINGS RULES 1955 GN NG**

**IN THE RM'S COURT/ DISTRICT COURT OF IGUNGA AT IGUNGA**

**CIVIL CASE NO. 1 OF 2022**

**ELIAS DOTTO JUSTINE ....................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**MICHAEL RAMADHAN MHANDO...............DEFENDANT**

**TO MICHAEL RAMADHAN MHANDO**

Take notice that the hearing of the above suit had been set down for MENTION day in the DISTRICT COURT Noon 8:30 am this 6th day of JUNE 2022 You must produce on that day all the witness open whose evidence and all the documents upon which you intend to support of your case

Given under my hand and seal on this court this **25th day of MAY 2022**

RESIDENT MAGISTRATE /DISTRICT
IGUNGA
RESIDENT MAGISTRATE
IGUNGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KILOSA**

**MAOMBI MADOGO NA.133/2021**

**JOHN NEHEMIA......................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ISAYA LEMBELE......WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA HASSAN .O. NYABWEDA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa, tarehe21/06/2022 mwenyewe binafsi au muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kusikilizwa.Endapo hautohudhuria,maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 24 mwezi wa 03 mwaka 2022

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI N NYUMBA (W)
KILOSA

---

## KUIFUNGUA KADI YA GARI

**COMFORT HOLIDAYS COMPANY LIMITED** anatangaza kuifungua kadi ya gari iliyokuwa imefungwa yenye namba za usajili **T 981 AWX** aina **MITSUBISHI FUSO** ,chasisi namba **FK618D521018,**taarifa imetolewa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI **ARU/ARU/RB/209317/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **JULIAN JOHN ICHULIKA** (msimamizi wa Mirathi) anatangaza kupotelewa kadi ya gari aina ya Nissan Dutsan - Pickup yenye namba za usajili **T449 AFH** iliyosajiliwa kwa jina la aliyekuwa mmiliki wa awali GOSBERT RWEYEMAMU KABANDA. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/206949/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0682825079.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RICHARD JOHN MBWAMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya TOYO yenye namba za usajili **MC 812 AJV,** chaasis namba **KE7KEFPK005837,** engine namba **162FMJC5118482,** yeyota atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/208628/2022**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Hivi kwa nini hawa watu wanatuona kama mimi na wewe ni mtu na mpenzi wake?" Lilikuwa ni swali la kwanza alilouliza Siwatu baada ya kufika shambani.

"Kwa sababu tunaongozana popote tunapokwenda." Bakari alijibu kirahisi.

"Nadhani siyo hilo tu."

"Lingine lipi Siwatu?"

"Ujue kwa sababu tunalala wawili tu mle kwenye nyumba yangu, wewe mtoto wa kiume na mimi wa kike, basi wanajua haiwezekani, kuna kitu kinaendelea tu mle ndani."

"Wangejua kuwa mimi nalala chini wewe kitandani..." Kabla hajamaliza, Siwatu aliangua kicheko kilichomfanya apaliwe na kukohoa.

"Du pole sana dada."

"Ahsante, ila umenichekesha sana leo." Akajibu baada ya kukohoa kupungua.

"Kwani uongo?"

"Kweli, ila si nakwambia lala kitandani hutaki."

"Hapana, wewe ni dada yangu na mtu ninayekuheshimu sana kwenye maisha yangu."

"Kwani si unalala tu nimekwambia, kwani ukilala ndiyo huniheshimu?"

"Mmmh, sitaki mimi, huko kulalalala huko..." Kabla hajamaliza Siwatu aliangua tena kicheko.

"Leo mgeni umeamua kunivunja mbavu tu."

"Si tumetengwa bwana, bora tuvunjane tufurahi, tuchekeshane wenyewe kwa wenyewe."

"Haya bwana, tukimaliza kupalilia, kachimbe mihogo, mimi nachuma kisamvu na majani ya kunde kwa ajili ya chakula, si unajua tena haturuhusiwi kununua chochote dukani?"

"Sawa, ila usijali, kama kunatakiwa vitu muhimu kama mafuta, sabuni, dawa ya mswaki, sukari, mchele, unga, nitakwenda kununua kwenye vijiji jirani na hapa."

****************************

"Mmmh, maajabu leo umekuja kunitembelea?"

"Maajabu gani, wakati mimi shoga yako Siwatu?

"Si mmeambiwa mnitenge msiongee na mimi, nyie?

"Mmmh, sawa, lakini shoga ni shoga tu, ndiyo maana nimeamua kujiiba, nimekuja kuongea na wewe."

"Ya kheri lakini Mage?"

"Tangu lini nikaleta uzandiki wakati mimi rafiki yako?"

"Haya, huyo shemeji yupo?" Akauliza Mage kwa kunong'oneza.

"Ndivyo mnavyoambizana huko kama huyu mimi bwana'angu, sivyo." Akauliza kwa sauti Siwatu alionekana ameanza kuchukia.

"Eeeh, basi samahani shoga kama nimeuliza vibaya, mimi ndivyo navyosikia kwa watu huko."

"Basi ukitoka hapa, kawaambie huyu ni rafiki yangu na wala si bwana angu kama mnavyofikiri. Na hayupo sasa hivi kaenda kijiji jirani."

"Eeeh, kufanya nini?"

"We Mage, fata ulichojia shoga."

Hakutaka kumwambia kuwa alifuata mahitaji ambayo kwenye kijiji hicho cha Semwanza walimzuia kuyapata.

Ilipita kama dakika tano hivi ya ukimya, ndipo Mage alianza stori zake.

"Nimekuja kukupa ujumbe wako kutoka kwa Maiko."

"Maiko gani?" Akauliza Siwatu kwa mshangao.

"Yule mtoto wa mzee Msemwa."

"Enhe anasemaje?" Akauliza tena.


"Anasema anakupenda sana, anakuhitaji uwe mpenzi wake."

"Mmmh!" Siwatu akaguna "Hivi hajawaona wanawake wengine kijijini kaniona mimi tu?"

"Siwatu, kila mwanaume ana mwanamke wake anayempenda, hebu angalia kaniacha mimi, anakutaka wewe. Kawaacha wote kijijini, anakutaka wewe. Hata mimi mwenyewe nimemshangaa. Kama uzuri hata mi mzuri mwenzangu, lakini kakutaka wewe tu."

"Sawa bibie, lakini nenda kamwambie, mimi sitaki na sina haja ya kuwa na mwanaume kwa sasa." Ni jibu ambalo lilimshtua Mage na kumshangaza.

Baada ya kuambiwa kuwa mgeni Bakari si mpenzi wake, basi alijua anaweza kukubali ombi la huyo aliyemtuma.




**"Siwatu, ukikataa sasa si watu watasema yule mgeni ndiyo mpenzi wako? Maana Maiko kasema yuko tayari hata kukuoa."**

"Mmh, sasa nikamwambieje?"

"Bibi wee, nenda kamwambie hivyo hivyo kama alivyokutuma. Simtaki."

"Siwatu, ukikataa sasa si watu watasema yule mgeni ndiyo mpenzi wako? Maana Maiko kasema yuko tayari hata kukuoa."

"Hahahaa" Siwatu alicheka kicheko cha hasira kilichochanganyikana na dharau. "Anioe mimi Maiko? Wapiii, yaani kabisa na akili zake, kakaa huko kafikiria, kakuita kakwambia nenda kamwambie Siwatu nampenda, tuwe wapenzi na ikiwezekana nitamuoa he he..."

"Basi, mimi nitamrudishia hilo jibu lake." Mage alijibu kwa upole na aibu.

"Tena kamwambie, anione kama chongo la mkwewe, akiniona asinisemeshe, wala kupita karibu na mimi. Kwanza nashangaa watu wamenitenga, wamenisusa, sasa yeye kilichomfanya ajishaue nini?"

"Sawa, sasa nimwambie ana mtu au?"

"Eee bibi wewe nawe usinitibue, niwe ninae niwe sina, haikuhusu, mlango ulioingilia ndiyo huo huo tokea. Kamwambie chochote kile, lakini simtaki. Na hili suala na kudhani kama itaonekana Bakari ndiyo mpenzi wangu mimi halinisumbui. Mbona wote kijijini wanajua kuwa ni mpenzi wangu wakati siyo." Siwatu alionekana kama vile amefikia kilele cha hasira.

"Eee, basi yameisha." Akajibu Mage huku akiinuka tayari kwa kuondoka.

"Asikutume tena, na wewe usikubali tena kutumwa na huyo mtu wako, tena kamwambie, iwe mwanzo na mwisho."

Siwatu alisimama mlangoni na kumuangalia kwa hasira na dharau Mage aliyekuwa anaondoka taratibu.

"Msichana usiyetaka kukaa kwako unamsaidia mama yako kufua au kupika, kazi kiguu na njia tu kwa umbea, lo..." Akaongea kwa sauti ya chini ambayo isingeweza kusikika na mtu yoyote zaidi ya yeye mwenyewe.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# KOCHA MBEYA KWANZA HAWEKI SILAHA CHINI

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Renatus Shija amesema kuwa bado wanaendelea kupambana kuondoka kwenye msitari hatari wa kushuka daraja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya timu yake hiyo kupata ushindi wa 2-0 kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, dhidi ya Kagera Sugar.

Kocha huyo ambaye anachukua nafasi ya Mbwana Makata aliyefungiwa kujihusisha na soka kwa muda wa miaka mitano, amesema yeye na wachezaji wake anaendelea kupambana na wanaamini kuwa watafanikiwa kujinasua.

"Tumepata ushindi na tunaendelea na mapambano. Mapambano yanaendelea, hakuna kuweka silaha chini na kusalimu amri," alisema Kaimu Kocha Mkuu huyo.

Mabao ya Mbeya Kwanza ambayo inautumia uwanja wa Majimaji uliopo mkoani Ruvuma kama uwanja wake wa nyumbani, yalifungwa na Eliuter Mpepo na Jimmy Shoji, yakiipatia pointi tatu ambazo zimeifanya kupanda nafasi moja juu ya Prisons ambayo pia ni Mbeya.

Timu hiyo imekwenda hadi kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi 24 sawa na Prisons inayoshika mkia kwa sasa.

Tofauti yao ni kwamba, Mbeya Kwanza imefunga mabao 20, huku Prisons ikifunga 18.

Hata hivyo, Mbeya Kwanza imebakisha mechi nne tu kumaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, huku Prisons ikibakisha mechi tano.

Timu mbili za chini zitashuka daraja moja kwa moja, huku ya 13 na 14 zitacheza mechi za mchujo na mshindi itakwenda kucheza na timu itakayoshinda mechi ya mchujo ya Ligi ya Championship.

Timu ya Ligi Kuu itakayoshinda, itabaki, na ikifungwa itashuka daraja, lakini ya Championship ikishinda inapanda Ligi Kuu, ikifungwa anabaki kwenye ligi hiyo ya Championship.




Mratibu wa onyesho la Wafia Dansi, Benard James (wa tatu kulia) akizungumzia onesho hilo katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam. Tamasha hilo linafanyika leo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mgunda atoa matumaini nusu fainali FA

**Na Cheji Bakari, TANGA**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema kuwa ana matumaini ya kuibuka na ushindi dhidi ya timu ya Azam FC katika mechi ya nusu fainali ya pili ya Kombe la FA.

Mchezo huo utachezwa kesho Jumapili katika uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Nusu fainali ya kwanza kati ya Simba na Yanga itachezwa leo Jumamosi katika uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili, Mgunda amesema kuwa wachezaji wake wote wapo tayari kwa ajili ya pambano hilo muhimu, hivyo matumaini ya kuibuka na ushindi ni makubwa.

"Wachezaji wa kikosi changu wote wapo imara, tumetoka mazoezini leo asubuhi (jana), nina matumaini makubwa ya kushinda mechi hiyo," alisema.

Kuhusu kiungo Mtenje Albano ambaye alikaa nje kwa muda wa trakribani miezi miwili baada ya kuumia kwenye mechi dhidi ya Azam kwenye Ligi Kuu, Mgunda alisema kuwa tayari ameshaanza mazoezi mepesi.

"Kwa upande wa Mtenje tayari ameshaanza mazoezi mepesi," alisema.

## Pambano la Mfaume lasogezwa mbele

**Na Saada Akida**

PAMBANO la kimataifa la bondia wa ngumi za kulipwa Tanzania, Mfaume Mfaume limesogezwa mbele hadi Julai Mosi mwaka huu.

Awali pambano hilo lilipangwa kufanyika Juni 10 mwaka huu katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam na limesogezwa mbele kwa sababu ya kupanga vizuri maandalizi.

Akizungumza na gazeti hili jana, muandaaji wa pambano hilo, Siah Moshi alisema kusogezwa mbele kwa pambano hilo ni kwa sababu ya kujiandaa zaidi kwa mtangane huo kuwa wa kiwango kikubwa.

"Kuna vitu havijakaa sawa hayo ni mambo yetu ya ndani hatuwezi kuweka hadharani, lakini Watanzania na wapenzi wa ndondi wategemee kuwa pambano lipo na kila kitu kinaenda vizuri na muda ukifika pambano litafanyika," alisema Siah.

Alisema ingawa pambano hilo limesogezwa mbele ila mabondia bado wanaendelea kujifua kikamilifu ili kuonesha mchezo mzuri siku hiyo.

"Mabondia wanaendelea na mazoezi yao licha ya kusogezwa mbele kwa pambano hili, pia tunahitaji kufanya pambano hili katika hali ya juu zaidi, "alisema Siah.

## Patric Kessy afyatua 'Heshima'

**Na Sabato Kasika**

MDAU wa muziki wa dansi nchini, Patric Kessy ameibuka na kibao kiitwacho 'Heshima' akiwa amemshirikisha rapa Greyson Semsekwa, kinachozungumzia kuporomoka kwa maadili ndani ya jamii.

Akizungumza na gazeti hili jana, mdau huyo alisema kuwa ameamua kutunga wimbo huo uliotoa mchango wake wa kukemea maadili mabovu ambayo yanazidi kushamiri na kuonekana ya kawaida.

"Nimeona nitoe mchango wangu kupitia sanaa, kwa wimbo huu ambao uko katika mtindo wa 'rhumba' nimemshirikisha rapa Semsekwa ili kukemea mmomonyoko wa maadili," alisema Kessy.

Mdau huyo ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mo Green inayojishughilisha na kilimo, alisema alianza kufyatua nyimbo miaka mitatu iliyopita na hivi karibuni alitoa huo mpya na tayari unasikika redio.

"Baadhi ya nyimbo zangu za nyuma ni 'Mwalimu, Siri, Dunia Kituo, Amenibamba na Afrika' ambazo ninaamini zina mchango mkubwa kwenye muziki wa dansi nchini," alisema.

Kessy alisema, nyimbo za muziki wa dansi zinaweza kuwa na mchango mkubwa kulinda maadili mema katika jamii, ambapo ameshauri wanamuziki kujikita katika utunzi wa nyimbo za aina hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE JONG NA MAN
KLABU ya Manchester United imemwambia kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, kwamba wataelekeza mawazo yao kwingine kama hatoweza kuamua kuhamia Old Trafford msimu huu wa joto. (***Sport***)

### TCHOUAMENI BASI TENA
PENDEKEZO la kiungo wa Monaco, Aurelien Tchouameni kuhamia Real Madrid limezuiliwa kutokana na suala la kodi. Mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wako tayari kulipa takriban euro milioni 80 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22. (***ESPN***)

### AURELIEN AGOMBEWA
KLABU za Manchester United, Liverpool, Arsenal na Chelsea zote zinamtaka Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 25 na watakuwa tayari kuingilia kati ikiwa uhamisho wake kwenda Real Madrid hautatimia. (Sun)

### LEAO NA MKATABA
KLABU ya AC Milan inataka kumpa mkataba wa muda mrefu, mshambuliaji wa Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 22. (***La Gazzetta dello Sport***)

### RICHARLISON KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Everton, Richarlison mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuondoka pale Goodison Park msimu huu wa joto huku Tottenham, Real Madrid na Paris St-Germain zikimhitaji mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. (***Mail***)

### CORNET AGOMBEWA
KLABU ya Everton inashindana na West Ham kumsajili mshambuliaji wa Burnley na Ivory Coast, Maxwel Cornet mwenye umri wa miaka 25. (***Telegraph***)

### KANE SAFI
NAHODHA wa Tottenham Hotspur, Harry Kane yuko tayari kufanya mazungumzo kuhusu mkataba mpya na klabu hiyo, licha ya mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 28 kushinikiza kuhamia Manchester City msimu uliopita wa joto. (***Evening Standard***)


### MKHITARYAN AWANIWA
INTER Milan wanatumaini kumsajili, Henrikh Mkhitaryan mwenye umri wa miaka 33 mara baada ya mkataba wake wa sasa na AS Roma utakapokamilika msimu wa joto. Kiungo huyo wa Armenia pia anafikiria ofa kutoka kwa washindi hao wa Ligi ya Europa Conference. (***Fabrizio Romano***)

### DOUCOURE AWINDWA
ARSENAL wanavutiwa na kiungo wa Lens, Cheick Doucoure mwenye umri wa miaka 22. Hata hivyo, Brighton, Everton, Crystal Palace na Wolves pia wanamfuatilia mchezaji huyo wa kimataifa wa Mali. (***Mirror***)

### EVANS KUPEWA MKATABA
KLABU ya Leicester City inajiandaa kumpa beki wa Ireland Kaskazini, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 34 mkataba mpya wa mwaka mmoja. (***Mirror***)

### NKUNKU HAKIELEWEKI
KLABU ya Manchester United inaweza kuwasilisha ofa kwa Christopher Nkunku anayelengwa na Liverpool na Chelsea wiki ijayo, huku mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24 akisita kusaini mkataba mpya na RB Lepizig. (***Florian Pettenberg, Sky Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE APANGA KUVUNJA REKODI YA ROONEY

## Ni kwa kupachika mabao mengi kwenye timu ya taifa ya England, asubiria kwa hamu kombe la Dunia na...

**LONDON,** UINGEREZA

HARRY Kane ana matumaini ya kuvunja rekodi ya Wayne Rooney ya ufungaji mabao kwenye michuano ya Kombe la Dunia baadaye mwaka huu, huku akitarajia kuwasaidia Simba Watatu hao kuimarika zaidi baada ya kutinga nusu fainali mwaka 2018.

Kane amefunga mabao 49 katika mechi 69 alizoichezea England baada ya kuifikia idadi ya Bobby Charlton katika mechi ya kirafiki dhidi ya Uswizi waliyoshinda 2-1 kwenye Uwanja wa Wembley, Machi mwaka huu.

Mshambuliaji huyo wa Tottenham Hotspur hivi sasa yuko nyuma kwa mabao manne pekee dhidi ya anayeshikilia rekodi, Rooney, licha ya kucheza mechi 50 chache zaidi za kimataifa kuliko gwiji huyo wa Manchester United.

Kane amekuwa na wastani wa mabao 0.71 kwa kila mechi kwa nchi yake, ikilinganishwa na Rooney mwenye wastani wa 0.45, na inaonekana kuwa suala la muda kabla ya nahodha huyo wa kocha Gareth Southgate kujitambulisha kama mfungaji bora zaidi katika historia ya timu ya taifa ya England.

Kane pia alifurahia msimu mzuri katika ngazi ya klabu, akifunga mabao 17 na kutoa asisti tisa katika Ligi Kuu England na kuisaidia Spurs ya kocha, Antonio Conte kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Akizungumza katika kipindi cha The Tonight Show, nyota huyo wa Spurs alielezea namna England ilivyojipanga bada ya kipigo chao cha nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018 kutoka kwa Croatia, huku akilenga kuvunja rekodi ya Rooney nchini Qatar.

"Nimefurahi," Kane alimwambia Jimmy Fallon mwendeshaji wa kipindi hicho.

"Katika Kombe la Dunia lililopita tulifika nusu fainali, ambayo ilikuwa ya mbali zaidi kuwahi kufika kwenye mashindano kwa miaka 30.

**"Nchi ilihamasika, lakini tuli pungua kwa hatua hiyo moja tu. Naisubiri kwa hamu hiv i sasa kwani tuna kocha mzur i na timu nzuri sana.**

"Tumekuwa tukijijenga vyema kwa Kombe hili la Dunia, na ninatumaini ninaweza kuvunja rekodi ya mabao tukiwa huko."

Kane anaweza hata kuvunja rekodi hiyo kabla ya michuano hiyo, huku England ikikabiliwa na mashindano manne ya Ligi ya Mataifa ya Uefa mwezi ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alifunga mabao sita wakati England ilipotinga hatua ya nne ya fainali za Kombe la Dunia lililopita nchini Urusi.

CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 1,000,0

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13


| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/05/22 | 17:00 | Hamarkameratene vs Odds BK | 2.43 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 28/05/22 | 17:00 | Ghazl El Mahallah vs Talaea El Gaish | 2.95 | 2.47 | 3.10 |
| 03. 28/05/22 | 18:00 | Mansfield Town vs Port Vale | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 28/05/22 | 19:30 | Smouha SC vs Enppi Club | 2.60 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 29/05/22 | 21:00 | Deportivo Madryn vs CA Guemes | 2.43 | 2.80 | 3.35 |
| 06. 29/05/22 | 02:00 | Toronto FC vs Chicago Fire | 2.50 | 3.45 | 2.65 |
| 07. 29/05/22 | 03:00 | Inter Miami CF vs Portland Timbers | 2.32 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 29/05/22 | 07:05 | Vissel Kobe vs Hokkaido Consadole Sapporo | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 09. 29/05/22 | 09:00 | Shonan Bellmare vs Cerezo Osaka | 3.20 | 3.15 | 2.28 |
| 10. 29/05/22 | 16:00 | Kuopion Palloseura vs HJK Helsinki | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 11. 29/05/22 | 18:30 | Huddersfield Town vs Nottingham Forest | 3.40 | 3.20 | 2.16 |
| 12. 29/05/22 | 19:00 | Molde FK vs Bodoe/Glimt | 2.26 | 3.65 | 2.85 |
| 13. 29/05/22 | 19:00 | FK Haugesund vs Aalesunds FK | 2.20 | 3.45 | 3.05 |
| 14. 29/05/22 | 19:00 | Sandefjord Fotball vs Kristiansund BK | 2.22 | 3.55 | 2.95 |
| 15. 29/05/22 | 19:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.25 | 3.45 | 3.00 |
| 16. 29/05/22 | 19:00 | Vaalerenga IF vs Rosenborg BK | 2.20 | 3.50 | 3.05 |
| 17. 29/05/22 | 21:00 | Coritiba FC PR vs Botafogo FR RJ | 2.32 | 3.15 | 3.10 |

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDINHO: MBAPPE ATAZIDI KUWA BORA



**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe tayari ni mchezaji bora wa Ufaransa na anaweza kuendelea kuweka historia baada ya kusaini mkataba wake mpya na Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa Ronaldinho.

Wiki iliyopita, Mbappe alikubali mkataba mpya wa miaka mitatu na mabingwa hao wa Ligue 1, akiitosa hadharani Real Madrid iliyokuwa ikimuwania kwa muda mrefu.

Mshambuliaji huyo aliyeshinda Kombe la Dunia mwaka 2008, alifunga mabao 39 na kutengeneza asisti 21 msimu huu, huku timu ya kocha Mauricio Pochettino ikitwaa taji la 10 la ligi katika historia yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 tayari ni mfungaji bora wa pili wa Ligue 1 katika historia ya PSG, akifunga mabao 171 katika mechi 217 za ligi akiwa na wababe hao wa Paris - Edinson Cavani pekee (mabao 200 katika mechi 301) ndiye anayemzidi.

Nyota wa zamani wa PSG Ronaldinho, ambaye alifunga mabao 25 katika misimu miwili akiwa na klabu hiyo kabla ya kutimkia Barcelona mwaka wa 2003, amesema Mbappe tayari anaonekana kuwashinda wachezaji wenzake Lionel Messi na Neymar.

"Kwa sasa, siku zijazo... ni mchezaji ambaye anaweza kuwa sehemu ya historia," alisema Ronaldinho akiiambia Mail Online.

"Anastahili heshima yote anayopata. Anaweka historia na anaweza kuendelea kutengeneza furaha kwetu katika mchezo huu.

"Leo ni mchezaji bora wa PSG. Kama angeondoka kwenda popote pengine, itakuwa tu kupata nafasi ya kuwa mchezaji bora katika nchi nyingine. Tayari yeye ni bora zaidi nchini Ufaransa.

"Paris Saint-Germain ina baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani kwa sasa - Messi, Neymar, Sergio Ramos.

"Baadhi ya wachezaji bora duniani wamo kwenye timu hii. Kwa hiyo, ikiwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani ataondoka, wachezaji wengine wa juu wataendelea kwenye nafasi zao."

# Mane kuamua baada ya Uefa

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane amesema atatoa jibu maalumu kuhusu hatma yake katika klabu ya Liverpool baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid itakayopigwa Paris, Ufaransa leo Jumamosi.

Barcelona na Bayern Munich zimehusishwa kumsajili Mane mwenye umri wa miaka 30 ambaye mkataba wake Liverpool utaingia mwaka wa mwisho Juni, 2022.

"Nimeweka umakini mkubwa kwenye mchezo wa Jumamosi, hilo ndilo jibu ambalo ni lazima nitoe kabla ya fainali," alisema Mane akinukuliwa na BBC Sport.

"Lakini mkirudi kwangu Jumamosi nitawapa jibu bora zaidi mnalotaka kusikia, kwa kweli. Ni jibu maalumu. Nitatoa majibu ya yote mnayotaka kusikia.".

Hata hivyo, Liverpool ina matumaini kumbakisha mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Senegal ambaye tayari ameshinda Kombe la Mataifa ya Afrika, kombe la Carabao na kombe la FA msimu huu.

00,000

# SHABIKI WA SIMBA, CHELSEA ASHINDA MAMILIONI

**Na Dennis Fussi**

MKAZI wa Mkoa wa Kagera, Baraka Lugwisha Shoki amejishindia kitita cha Sh 168,972, 500 baada ya kubashiri kiusahihi mechi 12 za mchezo wa Perfect 12 unaoendeshwa na kampuni ya M-Bet Tanzania.

Shoki ambaye ni shabiki wa Simba, Geita Gold FC na Chelsea alisema kuwa haikuwa kazi rahisi kwa yeye kushinda kiasi kikubwa cha fedha hicho kutokana na ugumu wa kubashiri kwa baadhi ya timu zilizokuwa zinacheza.

Alisema kuwa mechi iliyompa wakati mgumu ni kati ya Dodoma Jiji FC na Namungo FC iliyochezwa uwanja wa Jamhuri, Dodoma na Dodoma Jiji FC kushinda.

Alifafanua kuwa kabla ya mechi hiyo, Namungo FC ilikuwa na matokeo mazuri na Dodoma Jiji FC ilikuwa na matokeo mabaya na ilifanya mabadiliko ya benchi lake la ufundi. Alisema kuwa Namungo FC ilikuwa katika kiwango kizuri sana, lakini baada ya kuona Dodoma Jiji inacheza nyumbani, aliipa ushindi timu hiyo kwani isingekuwa rahisi kwao kuendelea kupoteza mechi hiyo.

"Baada ya Dodoma Jiji FC kuongoza, niliendelea kufanya maombi na nilitamani mwamuzi asiongeze muda kwani nilihofia Namungo FC wangesawazisha, hivyo nilichukia mwamuzi kuongeza dakika,"alisema Shoki.

Shoki ambaye ni mwalimu wa hesabu katika shule ya Sekondari ya Kikukwe, Bukob alisema kuwa atazitumia fedha hizo kwa kuongeza mtaji katika biashara zake na nyingine kuzitumia katika kilimo na kusomesha ndugu zake.

Meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi alisema kuwa ataweza kubadili maisha yake kupitia mchezo wao wa Perfect 12. Mushi alisema kuwa M-Bet itaendelea kuwa nyumba ya washindi kwa kuwazawadia mamilioni Watanzania.

Mushi pia aliwaomba Watanzania wenye umri zaidi ya miaka 18 kuendelea kubashiri kwani Mei 31 watafikia kilele cha droo yao ya Zali la M-Bet ambapo watatoa washindi watatu, mshindi wa gari aina ya IST, pikipiki na Sh milioni moja.

Alisema kuwa mpaka sasa wamewazawadia Watanzania pikipiki 12 na washindi wengine 12 wamejishindia Sh milioni moja kila mmoja.




Msemaji wa kampuni ya M-Bet Tanzania, David Malley (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa droo ya Perect 12, Baraka Lugwisha Shoki ambaye aliweza kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi 12 za ligi mbalimbali duniani na kufanikiwa kushinda Sh 168, 972,500. **PICHA: M-Bet**

# Zanzibar yapata usajili mchezo wa Drift

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KWA Mara ya kwanza Zanzibar imepata usajili wa mchezo wa mserereko wa magari (Drift) na sasa mashindano hayo yataanza rasmi visiwani humo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema kuwa mashindano hayo awali yalitarajiwa kufanyika Mei 26, lakini lilishindwa kufanyika kutokana na mchezo huo ulikuwa haujasajiliwa Zanzibar.

"Naomba sasa tuitaarifu dunia kwa mara ya kwanza Zanzibar usajili wa mchezo wa drift umesajiliwa rasmi, na kwa sababu mchezo huu umeshasajiliwa kihalali sasa tunajipanga kutekeleza mchezo huu na kuweka siku maalum ya uchezaji wake," alisema.

Alisema ili kuwa na Jumuiya ya mchezo huo lazima kuwe na Klabu na tayari klabu nne za Zanzibar zimeshasajiliwa ambapo Waziri mwenye dhamana ya michezo atakabidhiwa klabu hizo za jumuiya ya mchezo wa Drift.

Alisema mchezo huo utaongeza ajira nyingi za vijana, kupiga hatua za kiuchumi na kutimiza dhamira ya Mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Huu mchezo nchi za wenzetu upo ikiwemo Tanzania bara na ni mchezo kama ilivyo michezo mengine ilimradi kufuata kanuni zake,"alisema.

LIVE IN PLAY

PATA ODDS ZAIDI UKURASA WA KATI

MECHI KALI LEO

LIVERPOOL
VERSUS
REAL MADRID

1 | 2.04 X | 3.53 2 | 3.28

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 28/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1696 | Sofapaka vs Vihiga Bullets FC | 1.51 | 3.75 | 5.85 |
| 15:00 | 2182 | Dinamo Brest vs BATE Borisov | 7.78 | 4.77 | 1.31 |
| 15:00 | 2409 | Ulinzi Stars vs Bandari | 3.16 | 2.77 | 2.37 |
| 16:00 | 2085 | SC Salgueiros vs Leca FC | 2.37 | 2.72 | 3.21 |
| 16:00 | 2729 | IFK Goteborg vs GIF Sundsvall | 1.46 | 4.09 | 5.84 |
| 16:00 | 5309 | Vasteras SK vs Halmstads BK | 3.63 | 3.63 | 1.97 |
| 16:00 | 5917 | Mjallby vs Kalmar | 2.98 | 2.98 | 2.33 |
| 16:00 | 5930 | BFC Daugavpils vs FK Auda | 3.06 | 3.06 | 2.24 |
| 16:30 | 1421 | TEC vs Amsterdam FC | 4.30 | 4.30 | 1.57 |
| 16:30 | 4169 | Scheveningen vs Kozakken Boys | 2.25 | 3.55 | 2.67 |
| 16:30 | 5394 | Rijnsburgse Boys vs Jong Sparta Rotterdam | 2.02 | 4.09 | 2.78 |
| 16:30 | 5754 | Itijd Sterker Worden Hendrik vs Ido-ambacht-VV Noordwijk | 3.89 | 4.08 | 1.67 |
| 17:00 | 1112 | Inter Turku vs Ilves Tampere | 1.71 | 3.50 | 4.37 |
| 17:00 | 1156 | IF Vestri vs Thor Akureyri | 1.70 | 3.80 | 3.99 |
| 17:00 | 1574 | Ghazl EL Mahallah vs Talaea El Gaish | 2.99 | 2.46 | 2.99 |
| 17:00 | 1813 | Atyra FC vs CS 2 de Mayo | 2.17 | 2.97 | 3.31 |
| 17:00 | 2588 | Recreativo DO Libolo vs Bravos Maqui | 2.32 | 2.92 | 3.07 |
| 17:00 | 2691 | Kuando Kubango FC vs Sporting de Benguela | 1.55 | 3.70 | 5.45 |
| 17:00 | 2890 | CD Lunda Sul vs Sporting Cabinda | 2.22 | 2.92 | 3.26 |
| 17:00 | 3944 | Ham-Kam vs Odd Ballklubb | 2.04 | 3.44 | 3.39 |
| 17:00 | 4731 | AC Oulu vs Seinajoen JK | 3.17 | 3.21 | 2.11 |
| 17:00 | 5261 | Torpedo Zhodino vs Dinamo Minsk | 5.81 | 3.39 | 1.58 |
| 17:00 | 5433 | Haka vs Lahti | 1.76 | 3.46 | 4.09 |
| 18:00 | 1546 | BK Hacken vs Sirius FK | 1.41 | 4.47 | 6.02 |
| 18:00 | 4327 | Rudar Prijedor vs Zrinjski Mostar | 5.25 | 3.55 | 1.59 |
| 18:00 | 4792 | Mansfield vs Port Vale | 2.67 | 3.02 | 2.67 |
| 18:00 | 5805 | AFC Eskilstuna vs Ostersunds | 1.81 | 3.77 | 4.12 |
| 18:30 | 2743 | US Poggibonsi vs US Follonica Gavorrano | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 18:30 | 5296 | CA Progreso vs Uruguay Montevideo FC | 1.70 | 3.20 | 5.04 |
| 18:30 | 5875 | FS Metta/Lu vs SK Super Nova | 1.85 | 3.55 | 3.60 |
| 18:45 | 3965 | MC Alger vs JS Kabylie | 2.15 | 2.95 | 3.80 |
| 19:00 | 3495 | Shakhter Soligorsk vs Vitebsk | 1.42 | 3.99 | 6.82 |
| 19:00 | 3956 | CF La Nucia vs Arenas De Getxo | 2.05 | 3.11 | 3.45 |
| 19:00 | 4654 | Stromsgodset vs Viking | 3.23 | 3.53 | 2.08 |
| 19:00 | 5143 | Sestao vs CD Eldense | 2.57 | 3.05 | 2.61 |
| 19:00 | 5880 | FK Banga B vs Kedainiai Nevezis | 4.20 | 4.20 | 1.69 |
| 19:15 | 1027 | Lugo vs Malaga | 2.37 | 3.17 | 2.92 |
| 19:15 | 3899 | Amorebieta vs Ponferradina | 2.06 | 3.41 | 3.31 |
| 19:30 | 3601 | Smouha Club vs Enppi Club | 2.42 | 2.88 | 3.18 |
| 19:30 | 3844 | Tallinna Kalev vs Tallinna JK Legion | 2.49 | 3.22 | 2.58 |
| 19:30 | 5227 | Zamalek vs Ismaily SC | 1.75 | 3.14 | 5.38 |
| 21:00 | 1401 | Louisville City vs Tulsa Roughnecks | 1.57 | 3.89 | 4.87 |
| 21:00 | 2499 | Mushuc Runa vs Deportivo Cuenca | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 22:00 | 3913 | Nacional Potosi vs Blooming | 1.46 | 4.12 | 5.74 |
| 22:00 | 4673 | La Serena vs Audax Italiano | 2.77 | 3.11 | 2.39 |
| 22:00 | 4684 | Liverpool vs Real Madrid | 2.04 | 3.53 | 3.28 |
| 22:30 | 1182 | Goias vs Bragantino SP | 3.21 | 3.06 | 2.17 |
| 22:30 | 3710 | CSA AL vs Novorizontino SP | 2.16 | 2.87 | 3.46 |
| 23:30 | 1477 | Orense SC vs Guayaquil City | 1.60 | 3.71 | 4.88 |
| 23:30 | 2962 | CA Boston River vs Torque | 2.96 | 3.30 | 2.18 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumamosi Mei 28, 2022

Nipashe



## Kane apanga kuvunja rekodi ya Rooney



Peter Banda



Fiston Mayele

# KAZI MOJA TU LEO

### ●●●Mzizi wa fitina kukatwa wakati Yanga na Simba zikiingia dimbani kutafuta tiketi ya fainali ya FA, makocha watamba...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MZIZI wa fitina kwa watani wa jadi Simba na Yanga utakatwa leo, zitakapocheza mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

Timu hizo zimetoka sare kwenye mechi zote mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, hivyo ya leo itaamua nani mbabe msimu huu, kwani ni lazima mshindi apatikane.

Kama zitatoka sare ya aina yoyote, zitalazimika kupigiana penalti tano tano ili kumpata mshindi atakayetinga hatua ya fainali, ikizisubiri Azam FC na Coastal Union zitakazocheza kesho, kabla ya mechi ya fainali itakayochezwa Julai 2 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Timu zote mbili zitawakosa nyota wake muhimu kwenye pambano hilo, Simba ikiwakosa Shomari Kapombe, Jonas Mkude na Clatous Chama ambao ni majeruhi, huku kukiwa na hatihati pia ya kumkosa kipa wake namba moja, Aishi Manula aliyeumia kabla ya mechi dhidi ya Geita Gold Jumapili iliyopita.

Yanga nayo itawakosa wachezaji wawili muhimu ambao ni Saido Ntibazonkiza na Dickson Ambundo ambao wamesimamishwa na Kocha Mkuu Nasreddine Nabi kwa madai ya kutoroka kambini usiku na kurejea alfajiri mara baada ya mechi dhidi ya Biashara United Jumatatu iliyopita.

Kocha Mkuu wa Simba Pablo Franco amesema anakwenda kucheza mechi ngumu dhidi ya Yanga, lakini amewaandaa vijana wake vizuri.

"Mechi dhidi ya Yanga ipo mikononi mwa wachezaji wangu, kuhakikisha Simba inafikia malengo yake ya kupata ushindi na kusonga kwenye hatua inayofuata. Tupo karibu kulitetea kombe hilo, na mbali na mazoezi huwa nazungumza na mchezaji mmoja mmoja, hivyo tupo tayari," alisema.

Mmoja wa manahodha wasaidizi wa timu hiyo, Kapombe amesema wanaiangalia mechi hiyo kwa macho mawili kwa sababu Kombe la FA ndilo pekee kwa sasa wanalotegemea kulipata.

"Tumepata maandalizi ya kutosha, tunajua kama tumekutana nao kwenye ligi mara mbili, hii ni ya tatu, lakini hii ni tofauti kwa sababu inahitaji mshindi ili kwenda fainali. Sisi tumejiandaa kwenda fainali, ndiyo mchezo pekee tunaouangalia kwa macho mawili." alisema Kapombe.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga Nasreddine Nabi amesema tayari kikosi chake kimeiva kwa mazoezi waliyofanya Shinyanga ilikoweka kambi kwa ajili ya mechi hiyo.

Alisema kukosekana kwa wachezaji Ntibazonkiza na Ambundo hakuwezi kuathiri kikosi chake kwenye harakati za kupata ushindi kwenye mechi hiyo.

Yanga ilitarajia kuondoka leo hii hii Shinyanga, kuelekea jijini Mwanza kwenye mechi hiyo ambayo tayari imeteka hisia za mashabiki wa soka kwenye ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati.

Mara ya mwisho timu hizi kukutana kwenye mechi ya nusu fainali ya kombe hilo ni Julai 12, 2020 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikiibugiza Yanga mabao 4-1.

Msimu uliopita, timu hizo zilikutana tena kwenye kombe hilo, lakini safari hii ilikuwa ni fainali kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, Julai 25 mwaka jana, Simba ikishinda tena bao 1-0.

Kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, timu hizo zilikutana mara ya kwanza mzunguko wa kwanza Desemba 11 mwaka jana na kutoka suluhu bila kufungana, lakini matokeo kama hayo yalipatikana zilipocheza mechi ya mzuguko wa pili Aprili 30 mwaka huu.

# Ni fainali ya kisasi Liverpool, Real Madrid Ligi ya mabingwa

**PARIS, Ufaransa**

MIAKA 41 baada ya pambano lao la kwanza katika jiji zuri la Paris, Liverpool na Real Madrid wanakutana tena kaskazini mwa mji mkuu wa Ufaransa huko Saint-Denis kwa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, leo Jumamosi.

Wekundu hao wanaingia kwenye fainali hiyo wakiwa na mataji saba kwenye mashindano hayo, huku Los Blancos wakilenga kutwaa taji hilo kwa mara ya 14 katika historia yao.

Timu za Inter Milan, Benfica na Villarreal ziliondolewa na kikosi cha Jurgen Klopp kuelekea hapo kwenye uwanja wa Stade de France, huku vijana wa Carlo Ancelotti wakizitupa nje klabu kubwa Chelsea, Paris Saint-Germain na Manchester City.

Wakati Man City walikuwa na kazi kubwa ya kutikiswa na Aston Villa na Steven Gerrard kwenye mechi ya mwisho ya msimu wa Ligi Kuu England, lakini waliweza kulibeba taji hilo.

Liverpool washindi wa mataji mawili msimu huu walifanya kile walichohitaji kufanya na kufanikiwa kupata ushindi wa 3-1 katika siku ya mwisho ya kumaliza msimu wa Ligi Kuu England dhidi ya Wolves.

Lakini taji likabakia kwa vijana wa Guardiola ambao waliwaacha Liverpool kwa tofauti ya pointi moja.

Mechi hiyo ya leo Jumamosi itakuwa ni mara ya 10 kwa Liverpool kucheza fainali ya Ulaya.

Pia fainali hiyo ni marudio ya fainali ya mwaka 2008 wakati Real Madrid walilibeba taji hilo mbele ya Liverpool ambao walimpoteza nyota wao Mohamed Salah katika dakika za mwanzo kabisa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >